




UKURASA 5

**FISI** auawa akivamia kituo cha afya, wagonjwa ...




UKURASA 11



# Nipashe

Jumatatu Julai 11, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581003 *

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper FOLLOW US


## BARAZA LA EID

# PM atoa ujumbe mzito

**Aleleza** umuhimu watu kushiriki Sensa ya Watu na Makazi... *Endelea uk. 2*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza katika Baraza la Eid El Hajj, baada ya kushiriki swala iliyofanyika kitaifa kwenye Msikiti wa Mfalme wa Morocco Muhammad VI, Kinondoni, Dar es Salaam, jana. **Picha zaidi Uk. 18 PICHA: OWM**

UKURASA WA 3

## IDADI NDOGO MAHUJAJI YAMSHTUA RAIS MWINYI

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema idadi ya Waislamu wanaokwenda kushiriki ibada ya hija nchini Saud Arabia (Makka) wanaotoka Zanzibar, ni ndogo ikilinganishwa...

## MOI kutibu magoti teknolojia ya matundu bila mgonjwa kupasuliwa

UKURASA 10



Rais wa Zanzibar, Alhajj Dk. Hussein Ali Mwinyi, akitekeleza Ibada ya Suna ya kuchinja, baada ya kumaliza swala ya Eid El Hajj, iliyofanyika kitaifa Mkoa wa Kaskazini Unguja jana. Kushoto ni Mufti wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi na (wa tatu kushoto) ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Haroun Ali Suleiman na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud. **PICHA: IKULU**

# Wamiliki shule binafsi waiangukia serikali

UKURASA 2

**MICHEZO** **MSUVA KUFUNGA USAJILI YANGA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Prof. Godius Kahyarara (katikati) na viongozi wengine wa wizara na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya PSSSF na NSSF, wakimsikiliza Ofisa Mipango na Uwekezaji Mwandamizi PSSSF, Deogratius Marwa (kulia), walipotembelea banda la PSSSF kwenye maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PM atoa ujumbe mzito

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewasihi Waislam nchini, kuendelea kudumisha umoja, upendo ili kujiepusha na vitendo vinavyoashiria vurugu, uonevu na uvunjifu wa amani wanaposherehekea sikukuu ya Eid El Adha.

Alikuwa akihutubia Baraza la Eid El Adha, jana lililofanyika katika Msikiti wa Mfalme Muhammad wa Sita wa Morocco Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Aliwaasa kuendeleza mshikamano, utulivu ambavyo ni msingi wa kuwaweka pamoja wananchi, katika kujiletea maendeleo.

"Tunaposherehekea Eid El Adha ni vema pia tukakumbuka maneno ya Mtume Muhammad kwamba; "Mwenye kufanya maasi siku ya Eid ni sawa na kumuasi Allah Sub-hanahu Wata'ala siku ya kiama," alisema.

Pia Waziri Mkuu alisema Rais Samia Suluhu Hassan anawasihi Waislamu na Watanzania kwa ujumla kuendelea kuonyesha upendo, umoja na mshikamano hata baada ya kumalizika kwa masiku kumi bora katika mwaka yanayopatikana kwenye mwezi wa Dhul-Hijja.

"Nawahimiza tutumie fursa hiyo ya kuchinja kwa ajili ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fadhila mbalimbali alizotujalia pamoja na kuwahurumia na kuwaonyesha upendo wenzetu miongoni mwa maskini na mafakiri. Lengo ni kuhakikisha walionacho na wasionacho tunakuwa kitu kimoja na kufurahi pamoja," alisema.

SENSA

Aidha, aliwataka waumini kushiriki Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu.

"Tujitokeze kwa wingi kuhesabiwa na kuunga mkono zoezi hilo. Tutoe ushirikiano kwa makarani wa sensa na watendaji wetu wa mitaa katika kufanikisha," alisema.

Alimpongeza Shekhe Mkuu na Mufti wa Tanzania, Abubakar Zubeir bin Ally pamoja na Baraza la Waislam Tanzania (BAKWATA), kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuiunga mkono serikali katika utoaji na uboreshaji wa huduma mbalimbali za kijamii zikiwamo na elimu na afya.

Naye Shekhe Zubeir alisema sensa ni msingi mkubwa wa maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, na kuwaagiza mashekhe wa mikoa na wilaya kuendelea kuhamasisha waislamu nchini kujitokeza kuhesabiwa siku hiyo itakapofika.

"Suala la sensa ni jambo muhimu na linakubalika katika sheria za uislamu. Kama hakuna sensa hakuna maendeleo kwa sababu hata nyumbani kwako lazima uwe na sense, kama una watoto 13 utafuta unga na nyama ya kutosha watoto 13," alisema.

"Jitokezeni kuhesabiwa serikali inataka kujua idadi ya wananchi wake, ili iweze kupanga mipango ya maendeleo na utoaji wa huduma za jamii kwa wananchi wake kama afya, maji, umeme na elimu."

## Daraja la Wami kuanza kutumika Septemba

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

WASAFIRI wanaotumia Barabara ya Chalinze - Segera wanatarajia kufurahia usafiri kwa kupita katika daraja jipya la Wami mapema mwezi Septemba, mwaka huu.

Daraja hilo ambalo hadi kukamilika linatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 75, litaondoa kero ya ajali za mara kwa mara zilizokuwa zikisababishwa na wembamba ambao hauruhusu magari mawili kupishana kwa wakati mmoja.

Akizungumza mwishoni mwa wiki baada ya kutembelea daraja hilo kukagua maendeleo ya ujenzi, Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Pwani, Baraka Mwambage, alisema ujenzi umefikia asilimia 83.

Daraja hilo lilianza kujengwa mwezi Oktoba, 2018 na linatarajiwa kukamilika Novemba, mwaka huu na kuwezesha magari ya pande zote kupishana bila tatizo.

"Daraja hili lina urefu wa mita 510 na upana mita 11.85, mradi huu pia unajumuisha njia unganishi, magari yatakuwa yanapishana bila shida na miteremko yake imepunguzwa tofauti na daraja la awali wananchi wategemee kuanza kutumia daraja hili Septemba mosi," alisema.

Kadhalika, mafundi walioshiriki katika ujenzi wa daraja hilo wamenufaika na ujuzi mpya kutoka kwa mkandarasi na watautumia kujenga madaraja mengine hapa nchini.

Kuhusu ulinzi wa daraja hilo, Meneja alisema zipo kamera ambazo zitarekodi yote ikiwamo hujuma na vile vile, Tanroads watatoa elimu ya ulinzi kwa wananchi wanaoishi karibu.

Mhandisi wa daraja hilo kutoka katika kampuni ya China Power, Tumason Andrea, alimshukuru Rais Samia Suluhu kwa kutekeleza miradi mkakati na kutoa fursa kwa vijana kushiriki katika miradi hiyo na kuongeza ujuzi. Juma Mohamed ambaye ameshiriki kwenye ujenzi huo alisema ujenzi wa daraja la Wami umemsaidia kukua kiuchumi na kuongeza ujuzi mpya atakaoutumia katika miradi mingine.

Elizabeth Emmanuel, aliishukuru serikali kwa ujenzi wa daraja hilo ambalo litaondoa adha kwa watumiaji ambao wakati mwingine walikuwa wakikaa kwenye foleni kwa muda mrefu inapotokea ajali.

Said Sadick mmoja wa madaereva wanaotumia barabara hiyo, aliishukuru serikali kwa kuwaondolea adha za ajali kutokana na mteremko mkali na magari kushindwa kupishana kutokana na wembamba wa daraja.

Daraja la Wami lilijengwa mwaka 1959 katika miteremko mikali na kona kali likiwa na upana wa njia ya magari mita 3.6 na njia ya waenda kwa miguu mita moja na kutoruhusu magari kupishana na yanapokutana katikati hugongana na kutumbukia mtoni.

# Wamiliki shule binafsi waiangukia serikali

**Na Jenifer Gilla**

WAMILIKI wa shule binafsi nchini wameomba serikali kulegeza msharti kwa wanafunzi wa madarasa yenye mtihani wa taifa kuwapunguzia likizo itakayoanza Julai hadi Septemba, mwaka huu ili wajiandae na mitihani yao.

Aidha, wamesema wanatarajia kumwandikia barua Kamishna wa Elimu nchini, Dk. Lyabwene Mtahabwa, kuomba kibali cha kufundisha masomo ya ziada kwa madarasa yenye mitihani ya taifa (darasa la nne, saba, kidato cha pili na cha nne) katika kipindi cha likizo inayoanza mwezi huu wa Julai hadi Septemba, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Taifa wa Shirikisho la Wamiliki wa Shule na Vyuo Binafsi Tanzania (TAMONGSCO), Leonard Mao, alisema uamuzi huo umekuja baada ya maombi ya kwanza waliyopeleka kwa kiongozi huyo kwa njia ya simu kukataliwa.

Alisema alipozungumza naye kwa njia ya simu kiongozi huyo, alimpelekea maombi ya wadau wa shule binafsi kuomba kufundisha madarasa hayo, ili kuwaandaa vizuri katika mitihani yao kwa kuwa likizo hiyo ni ndefu tofauti na nyingine.

"Nilitumwa nipeleke maombi haya kwamba wamiliki hao wanaomba madarasa yenye mitihani ya taifa wapewe ahueni, maana hii likizo ni ndefu sana ina siku zaidi ya 35, badala ya kukaa moja kwa moja nyumbani watoto hawa wafanye 'remedial studies' (masomo ya ziada), ili muda wa mtihani ukifika wawe tayari," alisema Leonard.

Baada ya kupeleka maombi hayo Kamishna huyo, alimjibu kuwa wanafunzi hao waachwe wapumzike kwa kuwa wamekaa darasani kwa muda mrefu na serikali itachukua hatua kwa shule zote zitakazokiuka agizo hilo.

"Akaniambia, 'ninakuagiza waambie nchi nzima hawa watoto waende likizo kwanza kwa sababu wamechoka, kuanzia Januari mpaka mwezi wa saba wapo shuleni hawajapumzika, akili ya binadamu inahitaji kupumzika, kwa hiyo tusiwakandamize hawa watoto."

Walipopata majibu hayo, wadau hao wakajadili na kuafiki kuwa waandike barua, ili kutoa hoja umuhimu wa watoto hao kuhudhuria masomo kipindi hicho ikiwamo kuwapo muda mchache wa kujiandaa baada ya shule kufunguliwa.

"Kwa mfano darasa la saba wanaanza mtihani Septemba 9, na shule inafunguliwa Septemba 5, mwaka huu na wanatoka likizo wanaanza mtihani watakuwa wamesoma saa ngapi, wamefanya 'revision' (marudio) saa ngapi?"

"Tunachoomba ni kuwa waendelee na masomo kisha warudi nyumbani siku tatu kabla ya sensa, halafu warudi shuleni siku tatu baada ya sensa, kwa maana hiyo watahudhuria masomo wiki tatu na kupumzika wiki mbili badala ya kukaa nyumbani wiki zote tano," alifafanua Leonard.

Mwenyekiti huyo alifafanua kuwa lengo pia ni kuepusha wazazi kupeleka watoto katika shule zisizo rasmi na kuwaletea madhara, ikiwamo kufundishwa tofauti na miongozo ya shule au kufanyiwa vitendo vibaya hali itakayosababisha kufeli mitihani.

"Serikali iwe flexible (ibadilike), kama wazazi wanataka watoto wao wasome 'remedial' na washirikiana na walimu nini kinawazuia serikali kutoa ruhusa? Kwa hiyo wakishaniletea hiyo barua nitaipeleka mamlaka husika kisha tutasubiri majibu," alisema.

Nipashe ilimtafuta Kamishna wa Elimu Nchini, Dk. Mtahabwa, ambaye alisema wadau hao wanatakiwa wazingatie waraka wa mihula namba moja na mbili ambao unaelekeza watoto kupumzika katika kipindi hicho.

"Kwa hiyo tuzingatie nyaraka za serikali watoto wapate muda wa kupumzika, wao sio mashine, ni binadamu, maisha ya mtoto sio kupata alama A, maisha ya mtoto ni katika nyanja zote za ukuaji," alisisitiza Dk. Mtahabwa.

# Idadi ndogo mahujaji Zanzibar yamshtua Rais Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema idadi ya waislamu wanaokwenda kushiriki ibada ya hija nchini Saud Arabia (Makka) wanaotoka Zanzibar, ni ndogo ikilinganishwa na miaka ya nyuma kabla ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Akihutubia wananchi katika Baraza la Eid llilofanyika jana katika viwanja vya Chuo cha Amali Mkokotoni, Mkoa wa Kaskazini Unguja, alisema licha ya kupewa nafasi nyingi na serikali ya nchi hiyo kila mwaka, lakini watekelezaji wa ibada hiyo ni wachache.

Kabla ya Baraza hilo Dk. Mwinyi alijumuika pamoja na Waislamu katika ibada ya sala ya iddi iliyofanyika Kitoni, mkoani humo.

Alisema yapo baadhi ya mataifa ambayo nafasi wanazotengewa huwa hazikidhi mahitaji yao, jambo linalowafanya watu wenye nia na uwezo kusubiri kwa kipindi kirefu.

Alisema kwa mwaka huu Zanzibar imepewa nafasi ya kusafirisha mahujaji 11,476, lakini waliokwenda ni 1,559, idadi ambayo ni ndogo ikilinganishwa na nafasi iliyotengewa na Serikali ya Saud Arabia.

Kwa mujibu wa Rais Mwinyi, baadhi ya mahujaji hawakwenda kutekeleza ibada hiyo kutokana na kutokidhi kigezo cha umri, kinachotaka wanaosafiri wasivuke miaka 63 au sababu mbalimbali za kiafya na kuwataka kuendeleza kutia nia kwa sababu Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa kulipa waja wake kwa nia zao.

Aliwataka waislamu wanapokuwa na uwezo kwenda kutekeleza ibada hiyo ambayo ni nguzo ya tano katika uislamu wasisubiri kumaliza muda wao wa utumishi (kustaafu).

"Sikukuu hii ni neema nyingine aliyotupa Mwenyezi Mungu baada ya ile ya Iddi el Fitri ambapo leo tunaisherehekea baada ya waislamu wenzetu kutoka mataifa mbalimbali duniani kutekeleza ibada ya hija huko Makka Saud Arabia," alifafanua.

Alisema serikali inaendelea kukamilisha taratibu za muundo na sheria kwa ajili ya kuanzisha mfuko wa hija, ili kusimamia shughuli zote zinazohusiana na ibada hiyo.

Kadhalika mfuko huo utakuwa ni rahisi kwa wananchi kujiwekea akiba kidogo kidogo na kupokea misaada ya kifedha kwa waislamu wenye uwezo ambao watawasaidia wengine kwenda kutekeleza ibada hiyo.

Pia, aliahidi serikali kuzifanyia kazi changamoto zilizowasilishwa na mahujaji, ikiwamo kutafuta njia itayoiwezesha Zanzibar kuwa na akaunti yake ambayo itasimamia na kushughulikia miamala ya kifedha inayohusu shughuli za hija kwa upande wa Zanzibar.

Alisema itaendelea kutoa unafuu kwa tozo mbalimbali kwa mahujaji, ikiwamo gharama za vipimo vya UVIKO-19 kama ilivyofanya mwaka huu kwa mahujaji.

Alisisitiza kwamba wakati Waislamu wanasherehekea Sikukuu hii ya Idd el Adhha, ni muhimu kuhimizana wajibu wa kushirikiana katika kulinda na kudumisha malezi bora kwa watoto.

Dk. Mwinyi alisema kuwaandaa watoto kwa kuwapa malezi bora ni msingi muhimu katika juhudi za kuimarisha elimu, mapambano dhidi ya dawa za kulevya, vitendo vya rushwa, wizi na ufisadi, udhalilishaji na unyanyasaji pamoja na mambo yote yanayochangia mmomonyoko wa maadili ndani ya jamii.

Kuhusu sensa, alisema maandalizi yamefikia hatua nzuri na kazi kubwa ni kuelimisha wananchi umuhimu wa kushiriki kwa maendeleo.


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**THOMAS CHACHA ITINDE**
anatangaza ku[ potea kwa kadi ya gari aina ya **FUSO** yenye usajili namba **T 857 BRX.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**TAR/RB/612/2022**

216938502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**THOMAS CHACHA ITINDE**
anatangaza ku[ potea kwa kadi ya gari aina ya **FUSO** yenye usajili namba **T 725 CJS.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**TAR/RB/612/2022**

216938702

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**THOMAS CHACHA ITINDE**
anatangaza ku[ potea kwa kadi ya gari aina ya **PREMIO** yenye usajili namba **T 118 DGC.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**TAR/RB/612/2022**

216938602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JOHNSUNDAY ATHANASIA MBURUMA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **TOYOTA MARKX** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.599 DHR.** CHASSIS NAMBA **GRX1200946362.**YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **SON/MBO/RB/268416/2022**


# Sirro: Hakuna atakayesalimika kufanya uhalifu mtandaoni

**Na Frank Monyo**

MKUU wa Jeshi la Polisi Nchini (IGP), Simon Sirro, amesisitiza hakuna mtu yeyote anayeweza kufanya uhalifu kwenye mtandao asipatikane kutokana na jeshi hilo kujiimarisha zaidi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

IGP Sirro alibainisha hayo jana wakati alipotembelea banda la maonyesho la TCRA kwenye Viwanja vya Maonyesho ya 46 ya Biashara, jijini Dar es Salaam (DITF).

"Hakuna namna unaweza kufanya uhalifu mtandaoni na usipatikane na bahati mbaya utaadhirika kwa familia yako na jamii, kwa sababu utakamatwa tu, hivyo nawaasa sana Watanzania wenzangu tujiepushe na utapeli mtandaoni," alionya Sirro.

Alitoa wito kwa TCRA kutoa elimu zaidi kwa watumiaji wa huduma za mawasiliano akibainisha kuwa hiyo itakuwa ndiyo njia sahihi na muhimu zaidi ya kupunguza matukio ya uhalifu mtandaoni.

"TCRA najua wamejipanga na sisi Jeshi la Polisi pia tumejipanga, suala muhimu ambalo ningependa kuwashauri ni kwamba tuendelee kutoa elimu, tuna watu wetu wengine wanatenda uhalifu bila kujua kwamba ni uhalifu kwenye mtandao; hivyo elimu ni jambo la msingi sana," alisema Sirro.

Ofisa Mwandamizi Mkuu wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa Mamlaka ya Mawasiliano, Semu Mwakyanjala, alimweleza IGP Sirro kuwa TCRA imeendelea na jitihada ya kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi na salama ya huduma za mawasiliano na imeweka utaratibu wa watumiaji huduma hizo kwa njia ya simu kutoa taarifa ya uhalifu kupitia namba maalumu, na kuwataka watumiaji wote wa huduma hiyo kuhakiki laini za simu zilizosajiliwa kwa namba za Kitambulisho cha Taifa.

"Kamanda, TCRA tuna utaratibu unaomwezesha mtumiaji huduma za mawasiliano ya simu kutoa taarifa ikiwa atapokea ujumbe au simu ya utapeli kwa kutuma namba ya tapeli kwenda namba 15040, utaratibu huu tunautekeleza kwa ushirikiano na Jeshi la Polisi na watoa huduma, umesaidia sana kupunguza ripoti za uhalifu," alisema Mwakyanjala.

Watumiaji wa huduma za mawasiliano, alisema wanapaswa kuhakiki usajili wa laini zao za simu kwa kubofya *106# ili kusalia salama na kusisitiza kwa hatua hiyo inamwezesha mtumiaji kufuta namba asiyoitambua kupitia wakala wa mtoa huduma.

**Jeshi la Polisi pia tumejipanga, suala muhimu ambalo ningependa kuwashauri ni kwamba tuendelee kutoa elimu, tuna watu wetu wengine wanatenda uhalifu bila kujua kwamba ni uhalifu kwenye mtandao; hivyo elimu ni jambo la msingi sana," alisema Sirro.**






## Tunajenga Mustakabali Endelevu

Kwa kampuni ya Barrick, ujengaji wa mazingira endelevu unaanzia ndani kwenye uongozi wetu hadi kwenye bayoanuai, udhibiti wa majanga yanayosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa hadi kwenye jamii. Dhamira ya kampuni ya Barrick ya kuendesha na kuhakikisha biashara zetu ni endelevu na zinaendeshwa kwa uwajibikaji mkubwa ni sehemu ya vinasaba vyetu (DNA) ambavyo vinaakisiwa na jinsi kampuni yetu inavyozingatia uangalifu na umakini wa hali ya juu katika maeneo yetu ya uchimbaji wa dhahabu pamoja na shughuli zetu zote zinazofanywa katika maeneo yetu ya kazi.

BARRICK
www.barrick.com | NYSE : GOLD • TSX : ABX

Barrick Gold Corporation, inayo maeneo ya kazi katika nchi 18 na migodi 14 ya dhahabu. Uendeshwaji na uzalishaji wa migodi 6 kati ya hiyo ni wa viwango vya daraja la kwanza katika ngazi ya dunia (Tier 1 operations). Aidha kampuni hiyo inayo migodi mitatu ya uzalishaji wa madini ya kimkakati ya Shaba na inayo mipango ya muda mrefu ya kuhakikisha biashara hizi zinaendelea kuwa endelevu kutokana na rasilimali zilizopo.

216930802

# Mkenda awaonya viongozi usimamizi miradi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema hatasita kuwaondoa madarakani viongozi wa taasisi zilizo chini yake watakaoshindwa kusimamia kwa weledi utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi.

Prof. Mkenda alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki mjini Unguja, katika kikao cha viongozi na watumishi wa Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wakati wa ziara ya kukagua majengo ambayo ujenzi ulisimama kwa muda mrefu.

Alisema wizara haitavumilia taasisi yoyote iliyo chini yake inayofundisha wataalamu kushindwa kusimamia kazi inayopewa kwa weledi na kusababisha hasara kwa serikali.

"Nataka kuona taasisi zote ambazo zina jukumu la kuandaa wataalamu katika maeneo ya ujuzi na taaluma mbalimbali zikisimamia kazi zinazopewa kwa ubora na kwa viwango vinavyotarajiwa, hatutashindwa kuwaondoa viongozi wa taasisi ambao watashindwa kusimamia kwa weledi."

"Taasisi zinazopewa jukumu la kusimamia miradi ya serikali na hasa mradi huu wa HEET (Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi) ni lazima kuwe na weledi kuhakikisha kazi zinafanyika kwa wakati na kwa ubora, sina wasiwasi kuhusu utaalamu najua wapo tena tunawajua kwa majina, lakini kazi wanazozisimamia zikikosa ubora, hatutasita kuchukua hatua. Fedha za mradi huu ni mkopo hata kama riba yake ni ndogo bado Watanzania watalipa," alifafanua.

Alisema fedha za Mradi wa HEET zimeelekezwa zaidi kwenye kujenga ujuzi na ndiyo maana zimepelekwa kwenye taasisi zinazojenga ujuzi ikiwamo Sayansi za Bahari Zanzibar, ambayo inatoa mafunzo yanayojenga ujuzi katika nyanja mbalimbali za uchumi wa buluu.

Naye Mbunge wa Jimbo la Kiembesamaki, Mohamed Maulid, aliomba serikali kuangalia uwezekano wa kuwapatia meli ya mafunzo na wanaendelea kutumia ngalawa pamoja na meli za kukodi.

Awali, Mkurugenzi wa Taasisi ya IMS, Mosses Mbiru, alisema pamoja na ufinyu wa miundombinu, Serikali ya Muungano na ya Mapinduzi zimeendelea kutatua kero hiyo kwa hatua mbalimbali na Zanzibar ilitoa eneo la Buyu na ya Muungano ilitoa fedha kwa ajili ya kulipa fidia, kutayarisha mchoro, kupata mkandarasi pamoja na kuanza ujenzi katika eneo lenye ekari 123.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa (kushoto), pamoja na mkewe, Jennifer Bashungwa (katikati) wakiwa kwenye mazungumzo na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Shree Goverdhannathji Haveli hapa nchini, Yogesh Manek, walipohudhuria hafla ya ibada ya jamii hiyo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **Habari uk. 5 PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kuandaa majukwaa wanawake kukua kiuchumi

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema katika kudhibiti matukio ya ukatili nchini, serikali inaandaa majukwaa ya kujifunza namna ya wanawake kukua katika uchumi bila kuleta madhara ya ukatili kwa familia.

Alisema sababu za kuanzisha majukwaa hayo ni kutokana na kuwapo kwa kesi kubwa ya ukatili kwenye familia baada ya wanawake kufanikiwa kiuchumi.

Dk. Gwajima aliyaeleza hayo mwishoni mwa wiki, wakati wa Siku ya Vazi la Batiki ambayo ilifanyika jijini Dar es Salaam.

Pia alisema wanaandaa majukwaa ya kiuchumi kwa wanaume ili kuelimishana namna ya kuishi na wanawake waliofanikiwa kiuchumi bila kusababisha ukatili kwenye familia.

"Wanawake wamekuwa wazalishaji wakubwa wa uchumi, lakini kumekuwapo na matukio makubwa ya ukatili kwa sababu ya kufanikiwa kwenu, hivyo tunaandaa majukwaa haya muhimu ili tuelekezane namna nzuri ya kuishi pamoja na kudhibiti matukio haya kama sio kumaliza kabisa," alisema Dk. Gwajima.

Akizungumzia vazi la Batiki, alisema litawekewa viwango ili mtu yeyote duniani akilishika atambulike kuwa ni batiki kutoka Tanzania.

"Tunataka mahali popote vazi hili la batiki mtu akilishika ijulikane kuwa ni ya Tanzania kwa njia hiyo tutaweza kuwakomboa watu wetu na umaskini," alisema Dk. Gwajima.

Lengo ni kuwafikia watengenezaji wa batiki wakiwamo wanawake wengi waliojikita kwenye sekta ya biashara ndogo ili kila mmoja aweze kuinuka kiuchumi.

Alisema, Rais Samia Suluhu Hassan, alifungua fursa kwa wanawake na kuwaonyesha kuwa wanaweza na kwamba ni muhimu kuchapa kazi kwa kushirikiana na wanaume kuinua uchumi wa nchi.

"Kutungwa kwa Sheria ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2018 inayozitaka halmashauri zote kutenga asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo isiyo na riba, kwa makundi maalum ikiwamo wanawake imewasaidia wengi na mwaka 2020/21 zilitengwa jumla ya Sh. bilioni 62.68 na kufikia Juni 30, 2021, Sh. bilioni 53.81 zilikopeshwa kwa vikundi 7,993 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu sawa na asilimia 86," alisema Dk. Gwajima.

Alibainisha kuwa, kati ya fedha hizo Sh. bilioni 28.17 zilitolewa kwa vikundi vya wanawake 4,894 vilivyozalisha ajira 52,428.

Kwa upande wake Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe, aliwahimiza waandaaji wa Siku ya Batiki kufanyika nchi nzima.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Zainab Chaula, aliahidi kushirikiana na Katibu Mkuu wa Zanzibar kufanyia kazi maelekezo ya mawaziri hao.

# Vipaumbele 5 kumpeleka Makamba vijijini siku 21

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba anatarajia kufanya ukaguzi kwa siku 21 wa vipaumbele vitano vya wizara hiyo, ikiwamo usambazaji na upatikanaji wa umeme wa uhakika katika mikoa 14.

Pia atafanya ukaguzi wa shughuli za usambazaji wa mafuta, kuhakikisha kunakuwapo na uuzaji wa bei nafuu wa nishati hiyo katika maeneo ya vijijini na vitongoji na upatikanaji wa matumizi ya nishati safi na salama ya kupikia kwa wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Makamba alisema ukaguzi huo utahusisha pia wilaya 38 kwa kusimamia miradi inayotekelezwa na Wizara ya Nishati na taasisi zake.

Alisema maeneo ya vijijini wananchi wananunua mafuta aina ya dizeli na petroli kwa gharama kubwa, wengi wao wananunua mafuta kwenye chupa ambazo sio safi hatua inayoifanya wizara yake kutoa elimu kwa wananchi hao.

Waziri Makamba alisema ununuzi wa mafuta kwenye chupa ambazo sio safi kunasababisha vyombo vya moto yakiwamo magari na pikipiki kuharibika haraka.

"Tutazungumza na wananchi na kupokea kero, maoni, ushauri na kutoa majawabu, ufumbuzi na ufafanuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya nishati, ikiwamo vipaumbele vya wizara kwa mwaka wa fedha ujao," alisema Makamba.

Waziri Makamba aliitaja mikoa ambayo itafikiwa kuwa ni Mara, Mwanza, Geita, Simiyu, Kagera, Shinyanga, Tabora, Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Ruvuma na Mtwara.

Alisema mikoa mingine itafikiwa katika awamu zijazo zitakazofanyika kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Kadhalika, Waziri Makamba alisema kutafanyika shughuli ya uboreshaji wa huduma zinazotolewa na taasisi za Wizara ya Nishati.

"Lengo ni kusogeza huduma za wizara na taasisi zake kwa wananchi hususani kwa wananchi wanaoishi vijijini. Pia kuongeza uelewa kwa Watanzania kuhusu sekta ya nishati na mageuzi tunayofanya."

"Serikali hii inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan itahakikisha kwamba sekta ya nishati inachangia katika ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya Watanzania."

# Fisi auawa akivamia kituo cha afya, wagonjwa wataharuki

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANANCHI wa Kijiji cha Nandagala, Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, wamemuua fisi aliyevamia kituo cha afya na kusababisha taharuki kwa wagonjwa.

Wakizungumza na Nipashe, wananchi hao walisema fisi huyo ambaye amekuwa akihatarisha maisha ya wananchi kijijini hapo kila wakati, walimuua juzi baada ya kuingia kwenye Kituo cha Afya Nandagala.

Mlinzi wa kituo hicho, Ibrahimu Issaya, alisema siku ya tukio usiku akiwa kazini alipewa taarifa na uongozi wa kituo kuwa kuna gari la kubeba wagonjwa litafika kumchukua mjamzito kwenda hospitali ya wilaya kwa matibabu zaidi.

Issaya alisema baada ya taarifa hizo alifungua geti kwa ajili ya kuiruhusu gari hilo, kitendo kilichotoa mwanya kwa fisi hyo kuingia ndani bila yeye kutambua, hali iliyosababisha taharuki kwa wagonjwa na watumishi wa kituo hicho.

Alisema fisi huyo aligunduliwa na mmoja wa wagonjwa aliyekuwamo kituoni hapo na kutoa taarifa kwa mlinzi huyo.

"Huyu fisi inaonekana hakuwa mbali, hivyo wakati naruhusu gari kuingia ndani ya kituo, ndipo akatumia mwanya huo kuingia na kusababisha taharuki," alisema Issaya. Akisimulia zaidi mkasa huyo, mlinzi huyo alisema baada ya kuufunga mlango alifukuzana na mnyama huyo, huku akiomba msaada kutoka kwa watu wengine, ndipo wananchi wakajitokeza na kuanza kumshambulia fisi huyo.

Mmoja wa wananchi walioijitokeza kupambana na fisi huyo, Seifu Hamisi, alisema akiwa nyumbani kwake majira ya saa tisa usiku alisikia kelele za watu na kutoka nje kwenda kusaidia kupambana na fisi huyo.

"Nilipofika na kuingia ndani nikamuona yule fisi anakuja upande wangu nikampiga mshale mmoja, akatulia kidogo kisha nikamwongeza mingine tisa na kuanguka chini."

Alisema kitendo cha fisi huyo kuanguka chini kiliwafanya watu wengine waliokuwa na mapanga na mawe, kumshambulia hadi kufa.

Mussa alisema tukio la fisi kushambulia na kula watu wakiwamo watoto wadogo na wazee, limekuwa tatizo kijijini hapo.

Mganga Mfawidhi Kituo cha Afya Nandagala, Jamal Sadick, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo katika Kituo cha Afya Nandagala.

Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi Kata ya Nandagala, Pascal Mkilanya, naye alithibitisha kuawa kwa fisi huyo.

# Bashungwa ataja sababu wawekezaji kuvutiwa nchini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Innocent Bashungwa, ametaja uhuru wa kuabudu na amani iliyopo nchini kuwa ni miongoni mwa sababu zinazovutia wawekezaji kutoka nje ya nchi kuja kuwekeza.

Alikuwa akizungumza jijini Dar es Salaam, kwenye hafla ya ibada ya jamii ya Wahindi wa dhehebu la Shree Goverdhannathji Haveli, iliyofanyika mwishoni mwa wiki na kuhudhuriwa na wageni mbalimbali wakiwamo viongozi wa chama na serikali, mashirika na wawakilishi wa taasisi kutoka ndani na nje ya nchi.

Alisema kwa kutambua wawekezaji wengi wakubwa na wadogo wanatoka nje ya nchi na utamaduni wao na imani za dini tofauti, serikali imekuwa na jukumu muhimu la kuhakikisha inawapatia uhuru wa kuabudu na kuheshimu imani zao.

"Kutokana na hali hiyo wawekezaji wamekuwa wakija kwa wingi bila hofu ya kukosa uhuru wa kuabudu wala kuingiliwa kwa namna yoyote kwa kuwa hawaendi kinyume na sheria za nchi. Matokeo ya uwekezaji wao yamekuwa na tija kubwa kwa serikali kuu pamoja na halmashauri zetu kupitia kodi na ajira kwa wananchi waliopo kwenye maeneo ya uwekezaji," alifafanua.

Alisema kwa upande wa serikali, kupitia viongozi mbalimbali imekuwa ikitumia vyema matukio hayo kuhakikisha sio tu inaonyesha ushirikiano na jamii hizo za kigeni, bali pia kuwasilisha agenda mbalimbali za kiuchumi na maendeleo.

"Kwa kuwa matukio kama haya yamekuwa yakivutia sio tu washiriki kutoka ndani ya nchi bali pia wapo wengi wanaotoka nje ya nchi wanaokuja kuungana na wenzao katika ibada kama hizi hivyo inakuwa rahisi kwetu pia kupenyeza agenda zetu kwao," alisema na kuongeza:

"Tunawashukuru na kuwapongeza wana jamii ya Shree Goverdhannathji Haveli nchini kwa kutupatia heshima na fursa hii muhimu," alisema Waziri Bashungwa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Shree Goverdhannathji Haveli nchini, Yogesh Manek, aliishukuru serikali kwa kutoa uhuru wa jamii kuabudu bila kuingiliwa sambamba na kuwatanguliza viongozi wa dini kwenye masuala mbalimbali, ikiwamo maamuzi makubwa yanayohusu mustakabali wa taifa.

"Hii ni heshima kubwa na kupitia ushirikiano tunaoendelea kuupata kutoka serikalini na viongozi mmoja mmoja imekuwa rahisi pia hata kwa viongozi wa madhehebu na dini tofauti kushirikiana sisi kwa sisi kwenye matukio kama haya."

"Hii ni hatua nzuri zaidi sio tu kidini bali pia kiuchumi kwa kuwa inaongeza mvuto hata kwa wale waliopo nje ya nchi kutamani kuja na kuwa sehemu ya wana jamii wa Tanzania na hivyo kuchochea uwekezaji," alibainisha.

Manek alisema, jamii hiyo imekuwa mstari wa mbele pia kushirikiana na taasisi nyingine nchini katika kusaidia miradi mbalimbali ya kijamii ikiwamo ya miradi ya afya na elimu.

Tukio hilo la siku tatu limefanyika kwa mara ya kwanza jijini Dar es Salaam likiwakutanisha watu kutoka jamii na taaluma tofauti, kwa ajili ya kuonyesha talanta na upendo wao kwa Mungu wa jamii ya Wahindi anayefahamika kama Shree Krishna.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.
(Together we can build a better life)

## PUBLICATION OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

**PURSUANT TO REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS DISCLOSURE REGULATION, 2014 AND REGULATION 40(3)(a) OF THE FINANCIAL CONSUMER PROTECTION 2019.**

| | TZS | | USD | |
|---|---|---|---|---|
| **A. SAVINGS BANK** | | | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | | FREE | | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | | FREE | | FREE |
| 3. A/C Statement Charges | | | | |
| a) Monthly | | FREE | | FREE |
| b) Interm | | TZS 4,300.00 | | $ 5.00 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | | FREE | Up to 5000 | FREE |
| | | | Above 5000 | 0.26% |
| 5. Cash Deposit Charges | | FREE | | FREE |
| 6. Balance Confirmation certificate | | TZS 12,800.00 | | $ 6.00 |
| 7. A/c Closure charges | | TZS 12,800.00 | | $ 13.00 |
| 8. Activation of Dormat A/c | | TZS 5,100.00 | | $ 6.00 |
| **B. CURRENT ACCOUNT** | | | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | | FREE | | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | | FREE | | FREE |
| 3. A/C Statement Charges a) Monthly | | TZS 4,300.00 | | $ 5.00 |
| b) Interm | Fixed | TZS 4,300.00 | Fixed | $5.00 |
| | plus For each page | TZS 500.00 | For each page | $1.00 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | UPTO 25 MILLION | FREE | Upto 5000 | FREE |
| | ABOVE 25 MILLION | 0.11% | 5000 to 10,000 - | 0.26% |
| | | | Above 10,000 | 0.43% |
| 5. Cash Deposit Charges | UPTO 50 MIO | FREE | Upto 10,000 | FREE |
| | ABOVE 50 Million | 0.11% | > 10,000- | 0.26% |
| 5. Balance Confirmation certificate | | TZS 21,200.00 | | $13.00 |
| 6. Stop Payment Charges | | TZS 25,500.00 | | $13.00 |
| 7. Cheque Clearing Charges | | | | |
| a) Inward | | TZS 1,300.00 | | $1.00 |
| b) Outward | | FREE | | FREE |
| 8. Cheque Return Charges | | | | |
| a) Inward | | TZS 25,500.00 | | $13.00 |
| b) Outward | | TZS 25,500.00 | | $13.00 |
| 9. A/c closure charges | | TZS 21,200.00 | | $17.00 |
| **C. MOBILE BANKING CHARGES** | | | | |
| **1. Cash Withdrawal** | | | | |
| Upto 100,000 | | TZS 1,700.00 | | NA |
| 101,000 to 200,000 | | TZS 2,600.00 | | NA |
| 201,000 to 400,000 | | TZS 4,300.00 | | NA |
| 401,000 to 600,000 | | TZS 5,100.00 | | NA |
| 601,000 to 999,000 | | TZS 6,800.00 | | NA |
| **2. Funds Transfer/Mobile Wallet** | | | | |
| Upto 100,000 | | TZS 500.00 | | NA |
| 101,000 to 250,000 | | TZS 900.00 | | NA |
| 251,000 to 500,000 | | TZS 1,700.00 | | NA |
| 501,000 to 1,000,000 | | TZS 4,300.00 | | NA |
| 1,001,000 TO 10 Mn | | TZS 8,500.00 | | NA |
| **Mobile Banking Services** | | | | |
| A) Monthly Subscription Charges | | TZS 500.00 | | NA |
| B) PIN Request | | TZS 2,200.00 | | NA |
| **D. LOCKERS RENT YEARLY** | | | | |
| 1.SMALL | | TZS 296,700.00 | | NA |
| 2. MEDIUM | | TZS 508,500.00 | | NA |
| 3. BIG | | TZS 635,600.00 | | NA |

| **E. REMITTANCES** | TZS | | USD | |
|---|---|---|---|---|
| 1. TISS | | TZS 8,450.00 | EQUIVALLENT TO TZS 8450 | |
| **2. E Remittances** | | | | |
| Upto USD 1000 or Eq. TZS | | TZS 17,000.00 | | $ 9.00 |
| 1001 to 5000 | | TZS 20,400.00 | | $ 11.00 |
| 5001 to 10000 | | TZS 40,700.00 | | $ 22.00 |
| 10,001 and above | | TZS 84,800.00 | | $ 43.00 |
| **3. SWIFT** | | | | |
| **a) Swift Outward** | | | | |
| Upto 5,000 | | NA | | $ 39.00 |
| 5,001 to 10,000 | | NA | | $ 51.00 |
| above 10,000 | | NA | | $ 77.00 |
| **b) Swift Inward** | | | | |
| Upto 5,000 | | NA | | $ 11.00 |
| 5,001 to 10,000 | | NA | | $ 16.00 |
| above 10,000 | | NA | | $ 26.00 |
| **F. LOAN/ADVANCES RELATED CHARGES** | | | | |
| 1. Processing Charges | Upto 5 Mio - | TZS 21,200.00 | Upto 5,000 - | $85.00 |
| | 5Mio to 10 Mio - | TZS 169,500.00 | 5000 to 10,000 - | $170.00 |
| | 10 Mio to 25mio - | TZS 339,000.00 | Upto 20,000 - | $255.00 |
| | 25 mn to 500 mio - | 1.28% | 20,000 to 500,000 - | 1.28% |
| | >500mio--* (*minimum 7.5mio) | 1.06% | >500,000--* (*minimum 7,500) | 1.06% |
| 2. Documentation Charges | Upto 100 MILLION | FREE | !"#$%& Upto 50,000 FREE | |
| | >100 Mio (-Min 300,000) | 0.26% | >50,000 - (Min 150) | 0.26% |
| 3. Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - | TZS 21,200.00 | Upto 20,000 - | $255.00 |
| | 5 Mio to 10 Mio - | TZS 169,500.00 | 20,000 to 500,000 - | 1.53% |
| | 10Mio 25mio - | TZS 381,400.00 | >500,000--* (*minimum 9000) | 1.28% |
| | 25 mn to 500 mio - | 1.53% | | |
| | >500mio--* (*minimum 9mio) | 1.28% | | |
| 4. Inspection Charges | Upto 100 Mio - | TZS 21,200.00 | Upto 50,000 | $22.00 |
| | >100 mio - | TZS 42,400.00 | >50,000 | $43.00 |
| 5.Credit Reference Report Charges from D&B Tanzania | TZS | TZS 101,700.00 | | $43.00 |
| 6.Pre-payment penalty | Calculated as %ge pre-paid amount in the case of takeover of liability by other | 1.70% | of pre-paid amount in the case of takeover of liability by other | 1.70% |
| **G. Guarantees (Local & International)** | | | | |
| Bonds & Guarantees | ( Min TZS 75,000) | 1.02% | | 1.02% |
| Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | per quarter (Min TZS 75,000) | 0.43% | | 0.43% |
| **H. LETTER OF CREDIT** | | | | |
| **Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof)** | | | | |
| Opening commission | | NA | ( Min $ 200) | |
| LC amendment Commission | | NA | ( Min $50 max 350) | 1.02% |
| Swift charge for LC opening | | NA | | 0.34% |
| Swift charge for other message/amendments | | NA | | $34.00 |
| Extensions - Commissions | | NA | ( Min $200) | $34.00 |
| LC cancellation charges | | NA | ( Min $200) | 1.02% |
| Non payment of Bills on due date | | NA | Till Payment | 1.02% |
| **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | | | |
| Advising commission | | NA | | $119.00 |
| Confirmation Commission | | NA | ( Min $150) | 0.43% |
| Negotiating bills under LC | | NA | (Min $75+cuourier+int) | 0.43% |
| Reimbursement claim paid | | NA | ( Min$75) | 0.43% |
| Extensions - Commissions | | NA | ( Min $200) | 1.02% |
| Collection of Export LC | | NA | (Min $75+cuourier+int) | 0.43% |
| Amendments | | NA | | $64.00 |

**OTHER DISCLOSURES(VIAMBATANISHI)**

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. Base or Prime Lending Rate | 16 | 7 |
| 2. Maximum spread above Base or Prime Lending Rate | 5 | 5 |
| 3.Penal Interest | | |
| a. For non compliance on Terms of Saction | 3% p.a over regular rate of interest | |
| b. For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | 5% p.a over regular rate of interest | |
| 4. Deposit Rates | | |
| a. Current account | Nill | Nill |
| b. Savings bank deposit | 3.00% | 1.00% |

**i. Fixed Deposits of TZS**

| Amount in TZS | up to TZS 50 Million | Over TZS 50 Million | Above 100 Million |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 3.50% | 4.50% | 5.50% |
| 91-180days | 4.50% | 5.50% | 6.50% |
| 181-364 days | 5.50% | 7.00% | 7.50% |
| Above 1 year | 8.00% | 8.25% | 8.50% |

**ii. Fixed Deposits of USD**

| Amount in USD | up to USD 50,000 | Over USD 50,000 | Over USD 100,000 |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 1.50% | 2.25% | 2.50% |
| 91-180days | 2.00% | 2.75% | 3.25% |
| 181-364 days | 2.50% | 3.00% | 3.50% |
| Above 1 year | 3.00% | 3.50% | 4.00% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| JOHN CHARLES | GM-OPERATIONS | SIGNED | 06-07-2022 |
| SALMA MRISHO | HEAD TREASURY AND TRADE FINANCE | SIGNED | 06-07-2022 |
| KAUSHENDRA TIWARI | GM-CREDIT | SIGNED | 06-07-2022 |

216938402

Canara Bank (T) Ltd, Head Office Dar Es Salaam Branch,Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania , 2112532, www.canarabank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Timu zienzi majina yetu

**MPIRA** wa miguu ni mchezo maarufu, si Tanzania pekee bali dunia nzima. Umaarufu wa Ligi Kuu ya England (EPL) umevuka mipaka ya nchi hiyo, ambao ni faida kwa klabu kubwa za England.

Ukizungumzia mechi za televisheni, ni zile za EPL ndizo zinazoongoza nchini kwa mashabiki kufurika katika maeneo mbalimbali kila mechi zinapochezwa, tena nyingine hushuhudiwa usiku mkubwa.

Klabu kubwa za England zimekuwa zikitumia vizuri wingi huo washabiki hasa katika bara za Asia kwa kufanya ziara za maandalizi ya msimu mpya.

Ziara hizo mbali ya kuwa sehemu ya maandalizi ya timu, lakini hutumika kwa kuuza vifaa mbalimbali vya timu kama jezi.

Kutengeneza wigo wa washabiki si kitu kidogo wala cha mzaha. Ukifuatilia historia ya klabu nyingine za England na sehemu nyingine duniani utabaini kuwa zimetumia muda mrefu kutengeneza washabiki kutokana na ukweli kuwa kuna klabu nyingi huko kwao.

Nyingi ya klabu hizo zimeasisiwa karibu au zaidi ya karne moja iliyopita, na sasa zimekuwa taasisi kubwa, tena si tu katika kucheza mpira wa miguu, bali heshima ambayo zimejijengea.

Hapa Tanzania tuna klabu kongwe na zenye wafuasi wengi za Simba na Yanga. Klabu hizi za Dar es Salaam zimeanzishwa zaidi ya miaka 80 iliyopita. Kimsingi klabu hizi ni za aina yake, kwani zina hazina ya washabiki.

Wakati klabu nyingine zinafikiria na kujipanga kwa ajili ya kutengeneza wigo wa washabiki, zenyewe zina wafuasi wa kutosha. Wafuasi ni zaidi ya washabiki, kwani hao wameshaamini katika Yanga na Simba. Huwezi kuwabadili kutoka kushabikia timu hizo.

Hawa iwe ni wafuasi, washabiki au wanachama tu wao hawazitazami klabu zao katika mwelekeo mwingine zaidi ya ushindi. Kwao maendeleo katika klabu ni ushindi tu, iwe kiwango cha mchezo unaochezwa ni mbovu lakini kinatoa matokeo wao hilo si tatizo.

Hii ndiyo changamoto kwa klabu zetu hizi mbili na nyingine. Kimsingi kama Simba na Yanga zimejitengenezea zaidi wafuasi kutokana na sababu za kihistoria tu.

Tunasema historia kwa sababu sasa hivi ukikutana na mfuasi wa Yanga au Simba mwenye umri wa miaka 50 hawezi kukupa sababu yenye mantiki ni kwa nini alifikia kuipenda klabu anayoishabikia.

Kama hali ni hivyo kwa hao ambao wameishi duniani kwa nusu karne itakuwaje kwa vijana wenye miaka 20 au 30? Hao ndiyo kamwe hawawezi kukueleza kinagaubaga ni kwa vipi waliangukia kushabikia Simba au Yanga.

Ni vizuri wasajili wetu na hata waanzilishi wa Manchester United ya Tanzania wakafahamu kwa nini hiyo ya England imeitwa Manchester United, ile ya Hispania inaitwa Barcelona au ile ya Italia inaitwa AC Milan.

Jambo la kwanza ambalo tunatakiwa kufahamu ni kuwa majina kama Manchester, Barcelona, Madrid, Milan, Tottenham, Blackburn ni miji au vitongoji katika nchi hizo za Uingereza, Hispania na Italia.


Ajax Amsterdam ni klabu ya nchini Uholanzi. Lakini leo inaweza ikawepo Ajax Dar es Salaam kama tu kutakuwa na uhusiano wa moja kwa moja na Ajax Amsterdam.

Hivyo, klabu hizo mara tu zilipoanzishwa zilianza kuwa na washabiki katika maeneo yao kwa sababu majina tu yanawakilisha miji husika. Mbeya City au Musoma Shooting zina uhalali wa kujitengenezea washabiki katika miji hiyo kwa sababu hiyo niliyoitaja hapo juu.

Hapa kwetu tuna timu ambazo hazioni tabu kucheza mashindano zikiwa zimevaa jezi za Chelsea, Manchester City au Barcelona. Ni ulevi tu wa kutojua au kutaka kujua kwa nini Chelsea imefika hapo ilipofika.

Umefika wakati kwa Ofisi ya Msajili wa Klabu na Vyama vya Michezo nchini wakati wa kusajili klabu kuangalia zaidi ya malengo na madhumuni katika katiba za klabu zinazoomba kusajiliwa. Maana ya majina ya klabu husika nayo iangaliwe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba, wanahabari, hawakumtendea haki Makelele

**MIAKA** ya nyuma kulikuwa na makala na mijadala mingi ya watangazaji na wachambuzi kuzilaumu klabu hasa kubwa za Simba na Yanga, hasa pale wachezaji na makocha wao wa zamani wanapougua.

Klabu za Simba na Yanga zilikuwa zinabebeshwa mizigo isiyokuwa yao, kwa kuelezwa kuwa zimewatelekeza wachezaji au makocha wao wa zamani wanapoumwa.

Utashangaa kusikia eti mchezaji wa miaka ya nyuma wa Simba au Yanga ambaye baada ya hapo alikwenda kucheza soka kwenye klabu nyingine, lakini akianza kuumwa, au amelezwa hospitali, basi inaelezwa kuwa ametelekezwa na kwa nini haimhudumii.

Nakumbuka wakati kocha wa zamani wa Simba, James Siang'a akiwa mgonjwa, baadhi ya wachambuzi waandishi wa makala waliandika kuishutumu Simba kwa kumtelekeza.

Huyo nimetolea mfano tu, wapo wachezaji wengi na makocha ambao wanapatwa matatizo, lakini vidole zinaonyeshwa Simba au Yanga.

Nilishangaa, kwani Siang'a, baada ya Simba alikwenda klabu ya Express ya Uganda. Yenyewe haikunyooshewa vidole. Nami nikafanya uchunguzi wangu mdogo tu, nikaibuka na makala iliyozima tabia hiyo.

Nikaandika Simba na Yanga ni Taasisi au Kampuni kama zingine na haziwezi kumhudumia mfanyakazi ambaye hayupo kazini kwa muda huo, au amestaafu. Kama kampuni zimekuwa zinawatibua wafanyakazi waliopo na walioacha kazi kwa sababu mbalimbali, zingekuwa zimeshafilisika.

Mfanyakazi huwa anawekewa akiba yake au mafao na kampuni yake, basi. Akistaafu au kuondoka kampuni haihusiki kumhudumia akiumwa.

Sikukataa kama wafanyakazi wenzake wa zamani akimchangia, iwe kwenye magrupu au vyovyote vile, lakini kampuni huwa haihusiki.

Hata klabu hizi nazo zina mamia ya wachezaji waliozichezea tangu miaka ya 1960, hadi leo hii na hawapo kwenye timu. Na makocha pia. Kwa vyovyote haiwezi kuwahudumia. Pia hawa wachezaji waliokuwa wanalipwa, hawakucheza bure, hivyo hawana cha kuzidai klabu hizo. Somo likaeleweka. Lakini hivi majuzi klabu ya Simba imefanya jambo ambalo hili sasa inabidi lipigwe kelele.

Aliyekuwa mchezaji wao, John Makelele 'Zigzag' alifariki dunia Jumamosi ya Julai 2, hatukuona angalau kupewa heshima tu ya kupotiwa kwenye akaunti ya klabu hiyo.

Ndiyo, si wote, au wachezaji wote wa klabu hiyo wapostiwe, lakini wale waliofanya makubwa ilibidi wafanyiwe hivyo, ikiwezekana na zaidi, kwani sikusikia hata kutuma salamu za rambirambi. Sijui kilitokea nini, kwani viongozi wa zamani wa Simba bado wapo na wala hatukuwasikia kusema lolote, achilia mbali hawa wa sasa. Sikutegemea mchezaji kama Makelele ambaye ana rekodi ya kuinusuru Simba kushuka daraja kifo chake kupita hivi hivi tu kama aliyefariki ni mtu wa kawaida.

Nilipongeze Shirikisho la Soka Nchini (TFF) ambalo lilituma salamu za rambirambi na kaposti kifo cha mchezaji huyo aliyeitumikia pia timu ya taifa, Taifa Stars.

Niseme tu hapa nchini kuna tatizo la kutojali historia, au rekodi zilizowekwa na wachezaji waliopita. Hata hawa wa sasa walimaliza na yao yatamalizika tu. Ingekuwa Ulaya kifo chake kingekuwa ni habari kubwa. Fikiria mchezaji aliyefunga goli ambalo limeinusuru Manchester United, Chelsea, Real Madrid, yaani hadi wachambuzi wetu hapa wangemchambua, lakini huyu Mbongo wameshindwa kumpa thamani.

Japo wengi wana umri mdogo, lakini maana ya uchambuzi na uandishi ikiwemo wa michezo ni kufukua rekodi za nyuma. Soka ni mchezo wa rekodi, historia na takwimu Mtu ambaye Julai 23, 1988, alifunga bao la pili dhidi ya Yanga, lililoinusuru Simba kushuka hakupewa stahiki yake hata na klabu yake. Leo hii wanachama na mashabiki wa Yanga wangekuwa wanaitania Simba kuwa ingewahi kushuka daraja kama isingekuwa mtu huyu, Makelele. Na sijui kama ingekuwa imeshapanda au bado. Inawezekana ingekuwa imependa, lakini ingekuwa na rekodi ya kushuka ambayo watani zao wangeitumia kama fimbo. Huyu mtu ilitakiwa mashabiki wa kizazi cha sasa cha Simba wamfahamu.

Ilikuwa ni mechi ya mwisho wa ligi, Simba ilitakiwa lazima ishinde isishuke daraja na Yanga ilitakiwa sare tu ili itwae ubingwa.

Edward Chumila akaipatia Simba bao dakika ya 21, Issa Athumani akawasazisha dakika ya 36. Makelele alifunga bao la pili dakika ya 58, akiiwezesha timu yake kushinda mabao 2-1, akainusuru Simba kushuka daraja na Yanga ikakosa ubingwa, ambao ulienda kwa Coastal Union. Lakini si wachambuzi wala klabu yake iliyomuenzi. Rekodi aliyoiacha duniani haitofutika milele, ila hakutendewa haki.

# Kampuni Tembo Nickel kusaidia miradi elimu, afya ya mil. 207.8/-

**Na Mwandishi Wetu,** NGARA

KAMPUNI ya Tembo Nickel inakusudia kusaidia miradi 11 itakayojumuisha miundombinu ya madarasa, ofisi za walimu na madawati, baada ya kusaini Mkataba ya Makubaliano (MOU) ya miradi ya kijamii ya Sh. milioni 207.8 kwa mwaka 2022.

Akizungumza kabla ya kusaini makubaliano hayo mbele ya madiwani wa Wilaya ya Ngara, Meneja Mkaazi wa Tembo Nickel, Benedict Busunzu, alisema fedha hizo ni sehemu ya kampuni hiyo kurudisha kwa jamii (CSR), jambo wanalolifanya kabla ya kuanza uzalishaji na kutimiza kifungu cha 105 (1) cha Sheria ya Madini, kinachotaka kampuni zote za madini kuandaa mpango wa kurudisha kwa jamii (CSR), kwa kushirikiana na halmashauri husika.

"Mkataba huu unaonyesha ushirikiano, upendo na ujirani mwema mapema. Miradi iliochaguliwa inagusa sehemu muhimu sana kwenye maendeleo ya jamii," alisema Busunzu.

"Kwenye sekta ya afya kuna miradi mitatu ambayo ni kuboresha vituo vya afya, miundombinu pamoja na kutoa vifaa tiba na dawa, kutakuwa pia na mafunzo ya muda mfupi ya wahudumu wa afya wa ngazi ya jamii kutoka vijiji tisa," alisema Busunzu.

Alisema miradi itakayotekelezwa kwa fedha hizo imeibuliwa kwa mchakato shirikishi kati ya Tembo Nickel na vijiji pamoja na kata zinazohusika.

Kata zitakazoguswa na miradi hiyo ni Bugarama, Bukiriro, Muganza, Rulenge, Mbuba na Keza.

Alisema tayari Tembo Nickel imetumia Dola za Marekani milioni 1.5 (Sh. bilioni 3.4 bilioni) kwa kununua huduma na vifaa na kati yake Dola 125,673 (Sh. milioni 293 milioni) zimetumika katika Wilaya ya Ngara, kwa robo ya kwanza ya mwaka huu Januari hadi Machi, 2022.

Akizungumzua ajira, alisema mgodi huo utanufaisha wananchi wote wa Tanzania, na kampuni imekuwa ikitoa kipaumbele kwa wananchi wa Wilaya ya Ngara.

"Hadi wiki iliyopita tulikuwa na wafanyakazi moja kwa moja 111, kati yao 72 wametoka Ngara, kwa wafanyakazi wa muda tulikuwa nao 51 na wote wanatoka Ngara, tunahakikisha kazi zinazoweza kufanywa na wanaNgara, wao ndiyo wazifanye," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, William Bambala, aliishukuru kampuni hiyo kwa kusaini mkataba huo, na kuahidi yeye na madiwani wenzake watahakikisha wanafuatilia utekelezaji wa mkataba huo.

"Kwa namna tunavyopenda maendeleo ya wanachi wetu, tutahakikisha kwamba miradi hii inasimamiwa vizuri na inatekelezwa kwa wakati," alisema.

Kwa upande wake Mbunge wa Ngara, Ndaisaba Ruhoro, alisema ili kujenga miundombinu ya madarasa na zahanati walikuwa wakichangisha wananchi, lakini fedha zilizotolewa na Tembo Nickel zitapunguza mzigo kwa wananchi.

"Mgodi huu ni wa miaka 33, lakini kabla hata hiyo miaka hatujaanza kuihesabu sasa hivi wako kwenye maandalizi ya mgodi matunda tumeanza kuyaona, hii ni hatua kubwa," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ngara, Solomon Kimilike, alisema mkataba uliosainiwa utasaidia umarishaji wa huduma za afya na kuboresha elimu kwenye kata zitakazoguswa.

"Niseme tu kupitia mradi huu Ngara itafaidika sana, kwasababu mradi ukianza halmashauri itakuwa ikipata asilimia 0.3, fedha hiyo itakuwa sehemu ya mapato ya ndani ya halmashauri, itasaidia miradi mbalimbali kwenye maeneo yote ya wilaya na sio tu vijiji vinavyozunguka mradi kama ilivyo sasa hivi," alisema.

Kwa upande wa Diwani wa Kata ya Bugarama, Theofilda William, alisema kabla ya kusaini mkataba, Tembo Nickel, ilikuwa imeanza kusaidia vijiji vinavyozunguka mgodi.




Meneja Mkazi wa Tembo Nickel, Benedict Busunzu (kushoto), akibadilishana mkataba wa makubaliano na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, William Bambala, (kulia) ni Mbunge wa Ngara, Ndaisaba Ruhoro. **PICHA: MPIGAPICHA**

# Wananchi wavutiwa utendaji Rais Mwinyi

**Na Mwandishi Wetu**

JITIHADA zinazofanywa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi za kurudisha nidhamu serikalini, kuziba mianya ya rushwa na kutengeneza mazingira ya kuvutia wawekezaji, zimekonga nyoyo za wananchi waishio nje ya visiwa hivyo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kuhusu utendaji wa Rais Mwinyi, walisema katika kipindi cha miaka miwili ya utendaji wake, wameona mafanikio makubwa serikalini.

Kassim Masoud Ismail, mkazi wa Unguja na mfanyabiashara eneo la Mto wa Mbu mkoani Arusha alisema, Rais Mwinyi amefanikisha kudhibiti mianya ya uwizi na kuboresha mifumo ya ukusanyaji mapato ya serikali visiwani humo.

"Hatua mbalimbali ambazo Rais Mwinyi amekuwa akichukua na anaendelea kuzichukua zina faida kubwa kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Wazanzibar wote walioko ndani na hata nje ya Zanzibar," alisema Ismail.

Alimwomba Rais Mwinyi kuendelea kukaza buti kwa madai wapo wanaopinga maendeleo.

Naye Mwongoza Watalii jijini Arusha, Nasoro Majid Mloweni alisema, "Umakini na busara alizonazo Rais Mwinyi hasa kuwatumikia Wanzibar wote bila kujali dini zao, vyama wala maeneo wanayotoka imemwongezea heshima na imani kubwa wananchi na tunamwombea sana."

Mloweni alimpongeza pia kwa ukusanyaji wa mapato ya serikali ambayo awali yalikuwa yanapotelea mikononi mwa wachache ikiwamo wote wanaopiga makelele mitaani.

Mfanyabiashara Darajani Zanzibar, Dennis Njoka, alimwelezea Rais Mwinyi kama kiongozi mwenye dira na mwelekeo kwa sababu maisha na ushirikiano miongoni mwa wakazi wa visiwa vya Unguja na Pemba ni mazuri.

"Huyu Rais yupo kwa ajili ya kuwatumikia wananchi. Tunampenda kwa sababu anafanya maamuzi sahihi kwa manufaa ya Wazanzibari wote," alisema Njoka.

Naye Simtaji Zuberi Mahamud, alisema hatua ambazo zinachukuliwa na Rais Mwinyi ni za kupigiwa kongole na Wazanzibar wote kwa sababu zinalenga kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi na kijamii kwa manufaa ya wote.

Dk. Paskalis Mtegete, alimwelezea Rais Mwinyi kama kiongozi wa vitendo na kuvutiwa zaidi na azma yake ya kutaka Wazanzibar kuchangamkia fursa lukuki zilizoko kwenye mnyororo mzima ulipo kwenye uchumi wa buluu'.

"Kinachotakiwa hapa ni elimu na kuainisha fursa zote zilizomo ndani. Zanzibar imebarikiwa kuwa na eneo kubwa la bahari, fukwe na visiwa vidogo ambavyo vikitumika ipasavyo vitabadilisha maisha ya watu," alisema.

Dk. Mtegete, daktari wa binadamu na mwenyeji wa Mkoa wa Njombe, alisema Rais Mwinyi tangu achaguliwe mwaka 2022, alifanikiwa kuziba mianya mingi ya upotevu wa mapato ya serikali.

Hivi karibuni viongozi wastaafu wa Chama Cha Mapinduzi Zanzibar walitaka viongozi wastaafu kwenye chama na serikalini, kumuunga mkono Rais Mwinyi kwa hatua mbalimbali anazozichukua kujenga Zanzibar.

## Watumishi wakumbushwa uhusiano bora kazini

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIBU Tawala Mkoa wa Singida, Dorothy Mwaluko, amewataka viongozi wa taasisi za umma na binafsi mkoani hapo kujenga mazingira rafiki baina yao na watumishi wanaowaongoza ili kuongeza tija na uwezo wa kutoa huduma mbalimbali zitakazokidhi mahitaji ya wananchi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa wiki ya utumishi wa umma mkoani hapa, alisema watumishi wa umma na sekta binafsi wanawajibu wa kuwahudumia wananchi pamoja na kutambua miiko, mila na desturi za utumishi wa umma, ambazo zitasaidia kuongoza uhusiano mzuri katika kutekeleza majukumu yao.

"Ili wananchi waweze kuhudumiwa ipasavyo kiongozi wa taasisi ni lazima awe na mahusiano mazuri na watumishi anaowaongoza. Pia awe na utamaduni wa kuwatembelea watumishi wa chini yake na kujua changamoto zinazowakabili," alisema.

Mwaluko alisisitiza kuwa kutoa huduma kwa wananchi bila upendeleo au ubaguzi wanapokutana na changamoto ambazo zitakuwa juu ya uwezo wao wawakilishe kwenye mamlaka husika ili ziweze kutafutiwa majibu.

"Wapo baadhi ya viongozi wa taasisi za umma au binafsi hawapo karibu na watumishi wa chini yao. Mtumishi akifanya kakosa kadogo kiongozi badala ya kusaidia kutatua anatishwa na kuambiwa atachukulia hatua kali dhidi ya mtumishi huyo, tabia hii haijengi na haivumiliki kabisa," alisema Mwaluko.

Mwaluko alisema watumishi wanapashwa kusimamia sharia, kanuni na taratibu, lakini wakati mwingine busara zinatakiwa zitumike hasa ukizingatia binadamu ni mtu wa makosa.

Aidha, ameonya viongozi wa taasisi za umma na binafsi ambao hawajishughulishi na utatuzi wa changamoto zinazowakabili watumishi walio chini yao kitendo alichosema kinachochea watumishi kukimbilia ofisi ya Katibu Tawala Mkoa ambayo imegeuka kuwa kama kliniki.

Katibu wa Chama cha Walimu Mkoa wa Singida, Mwalimu Suzan Shesha, alimshukuru kiongozi huyo kwa kubuni na kuanzisha wiki ya utumishi wa umma ambayo itasaidia kubadilishana uzoefu na kuongeza hali ya utendaji kuwahudumia wananchi.

Suzan alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa mambo mengi mazuri anayowatendea watumishi, wakiwamo walimu kutatua changamoto mbalimbali ikiwamo ya kupandishwa madaraja.

# TBS yaonywa ucheleweshaji vibali

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, amesema hatovumilia vitendo vya ucheleweshaji wa vibali vya uthibiti ubora wa bidhaa za wafanyabishara, vinavyotolewa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), jambo linalowakwamisha kuzifikia fursa.

Akifungua maonyesho ya biashara ya nchi za Afrika Mashariki, yaliyofanyika viwanja ya CCM mjini hapa, mkoani Kagera na kukutanisha wafanyabishara na wajasiriamali waongeza thamani kwenye bidhaa zitokanazo na kilimo na mifugo, alisema ni muhimu jambo hilo kutiliwa maanani.

Wazri Mulamula alisema wapo wabunifu wanaongeza thamani kwenye bidhaa zao, lakini inawachukua miezi mingi kupata nembo ya TBS, jambo linalosababisha washindwe kushiriki maonyesho ya Afrika Mashariki au kuuza bidhaa zao nje ya nchi.

Alisema serikali imefungua milango kwa wafanyabiashara na kwamba taasisi na mashirika yanayochelewesha vibali vya wafanyabiashara wanashindwa kwenda na kasi ya serikali.

"Unakuta mtu anaongeza thamani mazao labda anatengeneza mafuta ya kupaka, nywele, batiki vikoi, vitenge, lakini kila akiomba nembo ya ubora kutoka TBS hapati kwa wakati fursa zikifika anapitwa hili halitavumiliwa na ninaenda kulishughulikia," alisema Mulamula.

"Wafanyabiashara wetu wanacheleweshwa sana na wanakosa kujitangaza kwa sababu ya taasisi zisizoenda na wakati hatutavumilia," alisisitiza Mulamula.

Aidha, alisema kuna matatizo mengine katika mipaka na kutozwa gharama kubwa ya malipo inayokuja kwenye maonyesho na kuwekewa vizuwizi.

Kwa mujibu wa Balozi Mulamula, ili kurahisisha matatizo hayo kwa wafanyabishara atashughulikia na kuimarisha mshikamano wa nchi za Afrika Mashariki kwa lengo la kukuza biashara kwenye maonyesho.

Kadhalika, kuwa mambo mengine hufanywa na watendaji wa ndani kuweka vikwazo zaidi kwenye vizuizi vya barabara na gharama za tozo, ukamataji wa mizigo na sheria kandamizi kwenye maeneo ya biashara.

Mratibu wa maonyesho hayo, William Rutha, alisema washiriki ni zaidi ya 350 kutoka nchi za Uganda, Rwanda, Congo, Kenya na Burundi, huku wakiipongeza serikali kwa kuthamini sekta binafsi kuandaa maonyesho hayo.

Alisema serikali ikipunguza vikwazo katika mipaka na barabarani kutakuwa na uwezekano wafanyabiashara wengi kuleta bidhaa zao katika maonyesho mbalimbali yanayofanyika nchini.



Mdhibiti wa Ubora wa Elimu Manispaa ya Singida, Seif Mzirai (wa pili kushoto), akizungumza na walimu wakuu, taaluma na maofisa elimu kata, kwenye kikao kazi ili kuboresha ufaulu wa darasa la saba mwaka huu, katika bwalo la Shule ya Msingi Tumaini mjini Singida mwishoni mwa wiki. **PICHA: ELISANTE JOHN**

# Wakulima pamba waidai CCU Bil. 2/-

**Na Daniel Limbe,** CHATO

BAADHI ya wakulima wa pamba wilayani Chato mkoani Geita, wameiomba serikali kuingilia kati malipo ya fedha Sh. 2,316,905,260 baada Chama Kikuu cha Ushirika Chato (CCU) kuwakopa na kushindwa kuwalipa kwa wakati.

Kampuni hiyo imedaiwa kukopa pamba kwa bei ya Sh. 1,900 kwa kilo na kuwashinda wanunuzi wa kampuni binafsi ambao wanalipa fedha taslimu kwa Sh. 1,600 baada ya kudai kuporomoka bei kwenye soko la dunia.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wakulima hao, Getruda Katemi na Erick Rabius, wamesema walilazimika kuuza pamba yao CCU baada ya kuwa na bei kubwa kuliko wanunuzi wengine na waliahidiwa kulipwa pesa zao ndani ya siku tatu jambo ambalo halijatekelezwa.

"Tunaiomba serikali itusaidie tulipwe fedha zetu tulizouza pamba kwa CCU...tuliwapa pamba kwa kuwakopesha baada ya kuahidi kutulipa pesa ndani ya siku mbili au tatu, lakini sasa ni zaidi ya wiki nzima hali inayotupa mashaka ya kupata pesa zetu," alisema Rabius.

"Mimi nilikopesha pamba yangu tangu majuzi nikiamini nitalipwa pesa zangu haraka ili nimpeleke shule mwanangu ambaye amefaulu kujiunga na kidato cha tano...ajabu hadi sasa sijalipwa na hata pesa za matumizi nyumbani kwangu sina...naomba serikali itusaidie tulipwe," alilalamika Katemi.

Akizungumzia malalamiko hayo, Mwenyekiti wa Chama cha ushirika Chato, Greon Chandika, amekiri kuwapo kwa baadhi ya changamoto zinazolalamikiwa na wakulima ikiwamo kukopa pamba na kuchelewesha malipo kutokana na mfumo mbovu wa kimtandao kwenye Benki ya TADB.

Huku akiahidi kulipa deni ndani ya siku nne zijazo, Kaimu Meneja wa CCU, Berino Msigwa, alitupia lawama baadhi ya kampuni binafsi ambazo zinafanya figisu kwa ushirika huo ili usiaminiwe na wakulima, kutokana na wanunuzi hao kukosa pamba baada ya kushusha bei kutoka Sh. 1,900 kwa kilo moja ya pamba safi hadi Sh. 1,600.

Mkaguzi ubora wa pamba kwenye Wilaya ya Chato mkoani Geita na Biharamulo, mkoani Kagera, kutoka Bodi ya Pamba nchini (TCB), Samwel Mdidi, alithibitisha wakulima kukidai CCU deni la zaidi ya Sh. 2,316,905,260 huku akitishia kukifungia ununuzi wa pamba mpaka hapo watakapomaliza kulipa deni hilo.

"Ni kweli chama cha ushirika Chato wanadaiwa fedha nyingi na wakulima wa pamba...tulikuwa tunakusanya takwimu za kutambua jumla ya deni lote na baada ya kulibaini tunatarajia kuwafungia kununua pamba mpaka hapo watakapolipa fedha zote za wakulima...na pia tunatarajia kuwapiga faini kwa kosa la kukopa pamba kwa kuwa ni kinyume na sheria za

# Waajiri watakiwa kushirikiana na OSHA

**Na Frank Monyo**

MKURUGENZI wa Habari (MAELEZO) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, ametoa wito kwa waajiri na wafanyakazi kutoa ushirikiano kwa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), ili kunufaika na ushauri na miongozo ya kitaalam juu ya uboreshaji wa mazingira ya kazi.

Alitoa wito huo jana alipotembelea banda la OSHA katika maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) yanayoendelea katika viwanja vya Saba Saba jijini Dar es Salaam.

"Nawaopongeza kwa kazi nzuri, watu wengi wakisikia OSHA wanakuwa na hofu, lakini naomba tuwaone kama marafiki wa sehemu zetu za kazi kwakuwa wao ndiyo wanaokuja kutushauri ni vitu gani tuvizingatie tukiwa kazini, ili tufanye kazi zetu na kurejea majumbani kwetu tukiwa salama," alisema Msigwa nakuongeza:

"Najua mnafika katika maeneo mengi na sasa mnajulikana kila mahali kwasababu kazi yenu inaonekana na watu wanaanza kutambua. Niwaombe Watanzania tuendelee kutoa ushirikiano ili majukumu haya yafanyike kikamilifu jambo ambalo ni muhimu sana kwani tukiwapa ushirikiano ndivyo wanavyoweza kutushauri na kutuongoza vizuri zaidi na hivyo tutapunguza sana athari zinazoweza kuwapata wafanyakazi katika maeneo yetu ya kazi."

Aidha, Msigwa aliwataka waajiri kushirikiana kikamilifu na OSHA kujenga mifumo madhubuti ya usalama na afya maeneo ya kazi, ili kuwa na uzalishaji endelevu na wenye tija unaokwenda sambamba na kujali afya za wafanyakazi.

"Wakati mwingine tunaangalia sana gharama zinazotumika katika kushughulikia masuala ya usalama na afya, lakini hatuangalii thamani ya kazi kubwa inayofanywa na OSHA kwenye maeneo yetu ya kazi, ni lazima tutambue kwamba tukiwa na wafanyakazi wenye afya njema watazalisha zaidi na tutaokoa fedha nyingi zinazopotea katika matibabu ya wafanyakazi wanaoumia au kuugua kila mara pamoja na zile zinazotumika kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wapya," alisema Msigwa.

Nao baadhi ya wanufaika wa OSHA walisema, "kupitia maonesho haya OSHA wametusaidia sana kwa kutupatia elimu na huduma mbalimbali, ikiwamo usajili wa maeneo ya kazi na vyeti vya kukidhi matakwa ya awali ya usalama na afya mahali pa kazi (compliance license) huduma ambazo pengine tungeweza kuzipata kwa gharama kubwa," alisema Bright Dickson Fue, ambaye ni mwajiri.

OSHA ni Taasisi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu yenye jukumu la kulinda afya na usalama wa wafanyakazi katika sekta zote hapa nchini, husajili maeneo ya kazi, kufanya kaguzi mbalimbali za usalama na afya.

## BRELA kuingia makubaliano TAKUKURU

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), anakusudia kuingia makubaliano na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ili kupata haki za kisheria kuingia kwenye mfumo wa kielektroniki wa wakala kupata nyaraka za usajili wa kampuni na leseni za biashara.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa, alisema hayo wakati akifungua kikao kazi baina ya wakala na TAKUKURU kilichofanyika mjini hapo.

Alisema BRELA inapokea barua sio chini ya sita kwa siku kutoka TAKUKURU zinazohitaji taarifa za usajili wa kampuni mbalimbali na kupokea wito mbalimbali unazowahitaji maofisa wa wakala kwa ajili ya mahojiano na kuhudhuria mahakamani kushuhudia taarifa za kumbukumbu hizo.

"Licha ya kikao hiki, lakini tumeona ni vyema nani muhimu kuwapo kwa rasimu ya makubaliano (MOU) baina ya BRELA na TAKUKURU tutakayokwenda kuijadili kwa dhamira ya kuleta umoja na mshikanamo kwa taasisi zetu katika kutimiza majukumu la kila siku," alisema Nyaisa.

Alisema BRELA kwa sasa imehama kutoka matumizi ya barua na nyaraka za karatasi na kuingia kwenye mfumo wa kielektroniki kuanzia masuala ya usajili wa kampuni na utoaji wa leseni za biashara.

Kutokana na matumizi mfumo wa kielektroniki kusajili na uhifadhi wa kumbukumbu za kampuni zilizosajiliwa na utoaji leseni ilionekana kuna umuhimu wa taasisi mbili hizo kuanzisha utaratibu wa kuwa na vikao vya pamoja kwa lengo la kupeana elimu na uelewa kuhusu utendaji kazi wa majukumu ya kila taasisi.

Alisema uwapo wa hati ya makubaliano kutahakikisha changamoto zilizoko zinatatuliwa na kumalizika na kuleta uimara na ufanisi wa taasisi hizo mbili, ushirikiano wa kiutendaji na sio kuteteresha taasisi.

"Mpango huu wa pamoja wa kutekeleza majukumu haya kumeleta ushirikiano wa karibu kati ya BRELA na TAKUKURU hususani upatikanaji wa taarifa za kuwezesha chunguzi mbalimbali," alisema Nyaisa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi wa Operesheni za Uchunguzi wa TAKUKURU, Simon Maembe, aliipongeza BRELA kwa hatua ya kuhuisha upatikanaji wa taarifa kidigitali kwa kuwa itaisaidia TAKUKURU na pia wadau wengine ambao wanahitaji taarifa mara kwa mara kutoka kwa wakala huyo.

Alisema kutokana na jukumu lao la uchunguzi mara nyingi wanahitaji taarifa nyingi zikiwamo za usajili wa kampuni na shughuli wanazofanya nchini.

"Huu utaratibu wa kuomba hizi taarifa una lenga kujua kama kampuni zimesajiliwa na kama wamesajiliwa ni kwa ajili ya kufanya shughuli gani, kujua nani hasa wanahisa kwenye hizo kampuni na pia nani ni wakurugenzi," alisema Maembe.

Alisema kwa sasa BRELA wameanza kuhama kwenye mfumo wa zamani wa kutuma barua kuhifadhi taarifa kupitia mafaili.

Takukuru inapojihitaji hizo taarifa huziomba kwa njia ya kisheria ya kuwasilisha maombi BRELA na yanafanyiwa kazi na baadaye kurudisha majibu.

"Awali, mfumo wa zamani umekuwa unachukua muda, lakini kutokana na teknolojia kukua sasa hivi BRELA taarifa zote hizo wameziweka katika mfumo wa kielekroniki," alisema Maembe.



Rais Samia Suluhu Hassan, akimkabidhi tuzo kutoka Hospitali ya CCBRT Mkurugenzi wa Biashara wa Kampuni ya Vodacom Tanzania Plc, Linda Riwa, aliyepokea kwa niaba ya asasi ya Vodacom Tanzania Foundation, ikiwa ni shukrani ya mchango wa shilingi bilioni moja waliotoa wakati wa ujenzi wa wodi ya wajawazito na watoto wachanga hospitalini hapo, hafla ya ufunguzi wa jingo ilifanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wahariri wapigwa msasa uhifadhi maliasili

**Na Maulid Mmbaga,** BAGAMOYO

WAHARIRI wa vyombo vya habari nchini, wametakiwa kuzipa kipaumbele habari za uhifadhi wa maliasili ili kupunguza athari zinazoendelea kutokea za mabadiliko ya tabianchi zinazosababishwa na shughuli za kibinadamu.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa semina ya kuwaongezea uelewa wahariri wa vyombo vya habari nchini, Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), Dk. Ellen Otaru, alisema bahari hizo zikipewa kipaumbele zitaelimisha jamii umuhimu wa kutunza maliasili na kukabili changamoto zilizoko kama kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu.

Alisema matokeo hayo yanatokana na ongezeko la watu na wanyama na kwamba zinahitajika mbinu mbalimbali, ili kupunguza athari za uharibifu wa maliasili na kuendelea kulinda hifadhi na vyanzo vya maji vinavyopatikana kwa manufaa ya wanyama na binadamu.

"Ili kuendeleza utunzaji mazingira tunawahitaji watunga sera katika ngazi mbalimbali kuanzia ya chini kwa maana ya watekelezaji na washauri, lakini mpaka ngazi ya taifa kuweka misingi wenzeshi na endelevu, kila kiumbe ni muhimu katika mazingira anapoishi," alisema.

Ofisa habari na mhamasishaji kutoka Mradi wa Tuhifadhi Maliasili, unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Watu wa Marekani (USAID), Adda Nyoya, alisema mradi huo unajihusisha na maliasili ikiwamo kuhamasisha uhifadhi wa mapito ya wanyamapori (shoroba).

Pia, kazi nyingine ya mradi huo ni kujengea uwezo mashirika binafsi, ili waweze kutekeleza kazi ya utunzaji wa shoroba, huku wakihakikisha taarifa sahihi za utafiti zinatolewa kuielimisha jamii utunzaji wa njia hizo.

"Huu mradi unafanya kazi pamoja na kujua kwamba tunalinda maeneo yenye shoroba, lakini na binadamu wanaoishi karibu na maeneo hayo, wanakuwa na kipato ili wasiende kufanya uharibifu hifadhini, pia tunafanya kazi na maliasili kuhakikisha wanakuwa na takwimu za kutosha ili kufanya maamuzi mazuri ya kulinda shoroba," alifafanua.

Alisema wanawaongezea uelewa wauzaji wa maduka ya nyamapori, ili kujua wanapataje bidhaa hiyo kwa kuzingatia njia sahihi.

Mtekelezaji wa shuhuli za Mradi wa Tuhifadhi Maliasili Dk. Elikana Kalumanga, alisema baadhi ya watu wanaoishi karibu na hifadhi au mapito ya wanyama, wamekuwa na kawaida ya kulinda shoroba kwa ajili ya kutunza vyanzo vya maji vilivyopo eneo husika vinavyowanufaisha wao na sio kwa sababu ya wanyama.

Alisema kumekuwa na malalamiko wanyama kuharibu mazao na kuhatarisha usalama wa watu kwenye baadhi ya maeneo kutokana na binadamu kuweka makazi, pamoja na kuendesha shughuli zao za kila siku katika sehemu zinazotumiwa au zilizotengwa kwa ajili ya hifadhi ya wanyamapori.

"Kama tunajua kuwa tuna wanyama nchini ni lazima tujue namna gani bora ya kuishi nao kwa kuwa bado tunawahitaji wanamchango mkubwa kwa taifa, ni muhimu kufikiria mahitaji yao muhimu, kunapotokea changamoto sisi tuna uwezo wa kuangalia njia mbadala tofauti na wanyama," alisema.

Alisema watu wanapuuzia na kutoona umuhimu wa 'buffer zone' eneo linalotenganisha hifadhi na makazi ya binadamu, bila kujua linasaidia kupunguza mwingiliano wa magonjwa kutoka kwa wanyamapori kwenda kwenye mifugo.

Mhadhiri kutoka Shule ya Uandishi na Mawasiliano kwa Umma, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM-SJMC), Dk. Abdallah Katunzi, alishauri wanahabari kuandika taarifa mbalimbali ikiwamo za uhifadhi maliasili, zinazobeba mtazamo unaosaidia kuongeza uelewa katika jamii ya utunzaji wa mazingira.

## Wakuu vyuo watakiwa kubuni miradi kiuchumi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imewaagiza Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC), kutumia kwa umahiri uwekezaji wa miundombinu na vifaa uliofanywa ili kubuni miradi ya kiuchumi ikiwamo ya kilimo kwa kutumia maeneo yao ya ardhi kuongeza mapato.

Agizo hilo limetolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, mjini hapa, wakati akifunga mafunzo ya siku nne kwa wakuu wa vyuo hivyo kutoka mikoa ya Tanzania Bara.

Alisema serikali imeamua kuvifufua vyuo hivyo na kuvifanyia ukarabati mkubwa wa miundombinu ili kutoa mafunzo ya kisasa na kwamba ni jukumu la wakuu hao kubuni mbinu za kuongeza mapato badala ya kusubiri fedha za serikali pekee.

Aliwataka kuwasilisha mpango kazi wa uanzishaji na utekelezaji wa miradi ya uzalizalishaji, ikiwamo ya kilimo kwa ajili ya wanafunzi kujifuza kilimo bora na kuongezea mapato ya vyuo.

"Kuna maeneo makubwa ya ardhi katika vyuo vyenu hakuna sababu ya kuacha maeneo hayo yakawa mashamba pori, yatumike kwa kilimo ambacho kitasaidia wanafunzi kujifunza kujikimu kimaisha watakapohitimu tofauti na kutegemea fani zao pekee," alisema Prof Nombo.

Alisema maeneo vilivyopo vyuo hivyo kuna fursa nyingi za kuanzisha miradi na uwekezaji akitolea mfano uanzishaji wa kiwanda kidogo cha kuchakata mafuta ya mawese Kigoma na zabibu Dodoma.

Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Munguli, Bernald Sekamba, akizungumza kwa kwa niaba ya wenzake aliishukuru serikali kwa kuwezesha mafunzo hayo yanayowajengea uwezo wa kuanzisha miradi.

## Wanafunzi UDSM kuchangamkia fursa PURA

WANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kitivo cha Sayansi ya Kilimo na Teknolojia ya Vyakula wanaosoma kozi Uchumi wa Kilimo, Maliasili na Biashara, wamesema wamejipanga kuchangamkia fursa zinazopatikana katika sekta ya mafuta na gesi.

Walisema hayo walipotembelea banda la Mamlaka ya Udhibiti wa Shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA).

"Tumekuja katika hili banda la PURA kwa ajili ya kujifunza yanayoendelea kuhusiana na vitu tunavyovisoma darasani kama kweli vinakuwa halisi kwenye maisha ya kawaida, na pia kuona kama tunaweza kupata fursa kutokana na shughuli mbalimbali zinazofanywa na mamlaka hii," alisema Omari Mrisho, akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya wenzake.

"Tumebaini kwamba zipo fursa ambazo hata sisi wanafunzi tunaweza kuzichangamkia kwenye sekta hii ya mafuta na gesi, kwasababu kupitia PURA, tumebaini zipo fursa za aina mbalimbali kulingana na kiwango cha elimu cha mtu. Siyo wahandisi peke yake, bali wanapata watu wa nyanja mbalimbali na sisi tupo tayari kuchangamkia fursa zitakazopatika kAfrika sekta hii na kwingineko." Alisema tatizo lililopo kwa watu wengi ni kuogopa kitu kabla ya kukifahamu na kwamba bado kunahitajika elimu kwa Watanzania kuhusu namna ya kuchangamkia fursa mbalimbali pamoja na kuthubutu.

Mkuu wa Kitengo cha Ushirikishwaji wa Wazawa na Ujumuishaji Wadau, Charles Nyangi wa PURA, alisema wamewaonyesha wanafunzi hao fursa mbalimbali zilizoko katika sekta hiyo ya mafuta na gesi na kwamba kazi iliyobaki ni kwao kuchangamka.

Alitoa wito kwa wanafunzi hususani wa vyuo kwamba soko la ajira katika sekta mbalimbali bado ni kubwa pamoja na biashara na kuwataka wasikate tamaa.

## Wazawa wafurahia fursa miradi mafuta, gesi

WAZAWA wameishukuru serikali kuwawezesha kupata fursa kwenye miradi ya mafuta na gesi, huku wakiipongeza Mamlaka ya Udhibiti wa Shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), kuendelea kuwashauri na kuwaunganisha na fursa katika sekta hiyo ikiwamo kampuni za kigeni.

Akizungumza kwa niaba ya kampuni za wazawa zinazoendesha shughuli zao katika sekta hiyo, mmoja wa vijana wanaofanya kazi kutoka kampuni hizo, Tumaini Abdallah, alisema awali wakati wanaingia katika sekta hiyo walikumbana na changamoto ya kushindwa kuaminiwa.

"Tunaishukuru PURA kwa kutusaidia kufika hapa tulipo, wamechangia kutunyanyua kwa njia nyingi ikiwamo kutushauri namna ya kufanya shughuli zetu na namna ya kujenga uhusiano na kampuni za kigeni na pia wamekuwa wakituonyesha njia namna gani ya kupata fursa kwenye sekta hii," alisema Abdallah.

"Tulivyoingia kwenye sekta hii, wawekezaji ilikuwa ni ngumu kutuamini sisi Watanzania kama tunaweza kufanya hizi kazi ilikuwa ni changamoto sana, lakini kwa kupitia mamlaka hii, walitusaidia kuwaaminisha na mpaka leo hii tunafanya kazi." Alitoa wito kwa kampuni na kwa vijana wengine kuacha kusita kuingia kwenye sekta hiyo kwa kuwa kuna fursa nzuri.

"Kampuni na vijana wengine ambao wanasita kuingia kwenye hii sekta wasiogope, kama una nia thabiti na kama una maono ya kufika sehemu fulani ni lazima uamini kwamba watu waliopo nyuma yako wanaweza kukusaidia kukufikisha kwenye hayo maono kama ambavyo imetokea kwetu. Na kwa sisi tuliopo hapa tunathibitisha kwa moyo mmoja kwamba PURA wamekuwa msaada mkubwa kutushika mkono sisi wazawa na kutufikisha hapa tulipo," alisema.

"Nawashauri vijana wenzangu na Watanzania wengine wanaotamani kuingia huku wasiogope kwa sababu kwa mfano kama kwenye kampuni yetu asilimia 40 tuliopo ni vijana na tunafanya vizuri."

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya PURA, Halfani Halfani, aliwataka wananchi kuwa wavumilivu na kuiamini serikali kwa juhudi zake inazozifanya katika kufanikisha miradi mbalimbali ya sekta ya gesi na mafuta.

"Kwa mfano katika mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG) ambao majadiliano yake yanaendelea, mambo ya msingi yameshakubalika, kwa hiyo endapo mradi utaanza kutekelezwa na kufanya kazi utaleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi kwenye taifa letu," alisema Halfani.

# Kampuni 8 China zaingia mkataba kuanzisha viwanda TZ

**Habari zote na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mkuu wa Kituo cha Biashara na Usafirishaji cha Afrika Mashariki (EACLC), Cathy Wang, amesema tangu kuanza kwa maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa Dar es Salaam (DITF), kampuni nane za China zimetia saini Mkataba wa Makubaliano (MoU) na kampuni za Tanzania ambazo zitauza bidhaa na kuanzisha viwanda vya kuuza bidhaa mbalimbali nchini.

Wang, alisema miongoni mwa bidhaa zitakazouzwa ni mashine ndogo za kuchakata mahindi kwa ajili ya kutengeneza unga wa ngano, ufuta, mchele, karanga na unga wa mahindi.

Alisema lengo la kusainiwa mikataba hiyo ni kuongeza mahitaji ya biashara kwa soko la nje na ndani.

Wang alisema kati ya kampuni hizo nane, moja imefunga mkataba wa kuanza kuagiza mafuta yanayojulikana kitaalamu kama 'cold steel coil'.

"Tayari tumewasiliana na watengenezaji nchini China ili kuanza kutengeneza bidhaa hizo ili ziweze kuletwa Tanzania hivi karibuni," alisema Wang.

"Maonyesho ya mwaka huu yamethibitisha kuwa mashine za kilimo zina uwezo sokoni na baada ya maonyesho tunakwenda kufanya tathmini kuona ni kiasi gani tumefanikiwa ili tuendelee kuleta bidhaa sahihi katika maonyesho yajayo." Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, alipotembea mabanda hayo aliipongeza China kwa kuleta bidhaa zinazovutia wateja wa Tanzania.

"Wizara yetu, kwa niaba ya wizara nyingine na serikali kwa ujumla tunafurahi kwamba bidhaa zinazoletwa hapa zinahitajika kwa ajili ya matumizi ya wakulima," alisema Ridhiwani.

Alibainisha kuwa uhusiano kati ya nchi hizo utaendelea kuimarishwa, kampuni zaidi za kigeni zinahitajika kushirikiana na sekta binafsi na serikali ili kupanua biashara nchini.

Mwakilishi wa kampuni ya Waw Sinoray, inayojihusisha na uunganishaji pikipiki za magurudumu matatu kutoka Kibaha mkoani Pwani, Ally Mrisho, alisema tangu maonyesho hayo yaanze wameuza maguta saba kwa wakulima.




Ofisa Masoko wa Kampuni ya Gf Trucks & Equipments Ltd, Poul Msuku (kulia), akielezea ubora wa mtambo wa migodini aina ya XCM kwa wachimbaji wa madini wadogo kutoka Geita, walipotembelea Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam kwenye viwanja vya Julius Nyerere jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MOI kutibu magoti kwa matundu bila upasuaji

TAASISI ya Mifupa na Tiba (MOI), imesema inafanya operesheni ya magoti kwa kutumia teknolojia ya kisasa kutumia matundu bila kupasua.

Daktari kutoka katika taasisi hiyo, Sharif Luwema, aliiambia Nipashe, wameanzisha operesheni hiyo baada ya kuona idadi kubwa ya wanaowapokea wakisumbuliwa na tatizo la magoti.

"Katika maonyesho haya mwaka huu, tumeleta huduma mpya ya operesheni ya magoti, miongoni mwa wagonjwa wengi ambao tumewaona hapa ni watu wenye shida na wanalalamika maumivu makali ya magoti," alisema Dk. Luwena.

Alisema kati ya wagonjwa hao, wengi wao walisema hata walipofika kwenye vipimo hawakugundulika na tatizo licha ya kuwa wanapata maumivu.

"Wengi wameenda kwenye hospitali na wakafanya x-ray na wakaambiwa kwamba hakuna shida na wengine pia hawajawahi kufika kwenye hospitali. Hao wote tunawaona hapa na tunawashauri kuonana na daktari na kufika katika kituo chetu Moi kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi yakinifu," alisema Dk. Luwena.

"Wanapokuja kwetu na tukawafanyia uchunguzi wa MRI, baada ya hapo tunawafanyia operesheni ya kisasa kwa kutumia teknolojia mpya ya kufanya operesheni bila kupasua goti. Hii inafanyika kwa kutoboa matundu kadhaa kwenye goti, tunaingiza kamera na vifaa vingine vya operesheni, mgonjwa anakuwa anaona shida yake wakati wa operesheni hiyo na baada ya hapo anatembea bila shida tena ya maumivu kama ilivyokuwa awali."

Aliwashauri Watanzania kwenda kufanya uchunguzi haraka pale wanaposikia maumivu kwenye magoti kabla tatizo halijawa kubwa.

"Nawashauri Watanzania ambao wako Dar es Salaam na nje ya mkoa huo wafanye uchunguzi haraka wanapopata maumivu na kwa sasa watembelee katika banda letu Sabasaba na waonane na madaktari ili wapate ushauri na wahudumiwe kama inavyotakiwa," alisema Dk. Luwena.

Tatizo la magoti, alisema linaongezeka kadri ya siku zinavyokwenda na asilimia kubwa ya watu wanaowapokea ni wenye umri mkubwa na wengine kutokana na ajali.

"Wengi tunaowapokea ni wale ambao umri umeenda kuanzia miaka 55 na zaidi na tunawaona na tunawapatia huduma hiyo kwa kutumia teknolojia hiyo ya kisasa ya operesheni ya matundu," alisema Dk. Luwena.

Alisema kwa siku wanapokea wagonjwa zaidi ya 20 wenye shida ya magoti na wanaofanyiwa operesheni kila siku ni wawili mpaka watatu kwa siku.

"Dalili za mtu mwenye tatizo kwenye goti ni maumivu makali, kadri siku zinavyoongezeka maumivu yanazidi kuwa makubwa na hufika wakati mtu anashindwa kuchuchumaa na akichuchumaa anashindwa kuinuka, au akitembea umbali mrefu anasikia maumivu makali," alisema Dk. Luwena.

"Ikifika stage goti linashindwa kukunja na ukilazimisha kukunja unasikia kama sauti ya vitu vimesigana, hizo ni dalili ambazo wengi wanakuja nazo. Lakini kuna zingine ambazo kadri muda unavyozidi kwenda unakuta goti linavimba, linakuwa jekundu na hiyo ni stage ya mbali zaidi ila za mwanzoni mara nyingi ni maumivu."

Alisema athari kwa wasiotibiwa mapema ugonjwa huo wa magoti ni kubwa.


"Athari ni kubwa sana na ndiyo maana tunakuja sehemu kama hizi ili kuwaelimisha watu wawahi kutibiwa mapema kwa sababu kadri siku zinavyokwenda ndivyo tatizo linavyozidi kuwa kubwa, mifupa ya goti inaanza kusigana na ikianza kusigana inaanza kulika na tunakuwa hatuna tena uwezo wa kufanya oparesheni za kawaida, isipokuwa tunatakiwa tufanye kubwa zaidi kama vile kubadilishiwa goti lote na kuwekewa la bandia."

"Nasema ni operesheni kubwa kwa sababu ni ya kufungua magoti na pia ina gharama kubwa ambayo ni zaidi ya Shilingi milioni tano hadi 10, ndiyo maana tunawaambia watu waje mapema ili wakigundulika wafanyiwe operesheni ya kawaida ya kutumia matundu."

Nipashe
Spotika



NAMNA STERLING ATAKAVYOFITI CHELSEA UK. 12



# WACHEZAJI 10 ENGLAND WALIOCHEZA MECHI NYINGI ZAIDI KOMBE LA DUNIA

**LONDON, England**

ENGLAND wana historia kubwa katika Kombe la Dunia la Shirikisho la Soka la Kimataifa, FIFA. Kweli, kwa upande wa ushiriki wameshiriki mara 15 hadi sasa.

Lakini bado, ushindi wao mkubwa ni mara moja tu zaidi ya nchi nyingi, na wana wachezaji ambao wamejitokeza kwa Three Lions hao kwenye jukwaa la kimataifa na kuwa miongoni mwa wachezaji bora zaidi waliowahi kucheza mchezo huo.

Hawa ndio wachezaji kumi waliocheza mechi nyingi zaidi kwa England kwenye Kombe la Dunia.

**10. Chris Waddle**

Mechi za Kombe la Dunia: 11

Ushiriki wa Kombe la Dunia: 1986, 1990

Jumla ya mechi za England: 62

Mchezaji wa zamani wa Newcastle na Tottenham, Chris Waddle aliichezea England mechi 11 kwenye Kombe la Dunia.

9. Gary Lineker

Mechi za Kombe la Dunia: 12

Ushiriki wa Kombe la Dunia: 1986, 1990

Jumla ya mechi za England: 80

Kwa hakika Gary Lineker alikuwa mwanasoka mzuri siku hizo. Alicheza hata mechi 12 kwenye Kombe la Dunia, ingawa alijisaidia kwa bahati mbaya katika moja ya michezo hiyo, kwa hivyo ni nani wa kusema ikiwa hiyo ni muhimu?

**8. Michael Owen**

Mechi za Kombe la Dunia: 12

Ushiriki wa Kombe la Dunia: 1998, 2002, 2006

Jumla ya mechi za England: 89

Katika ulimwengu mwingine, Michael Owen angemaliza maisha yake ya uchezaji England kama mfungaji bora na mtengenezaji wa mechi. Kwa bahati mbaya, majeruhi yalipunguza siku zake za kucheza, lakini bado alifanya vizuri sana na Three Lions hao.

**7. Steven Gerrard**

Mechi za Kombe la Dunia 12

Ushiriki wa Kombe la Dunia: 2006, 2010, 2014

Jumla ya mechi za England: 114

Stevie Gerrad ni mmoja wa wachezaji wachache walioshiriki katika timu zote za 'kizazi cha dhahabu' chini ya makocha, Sven-Goran Eriksson, Fabio Capello na Roy Hodgson.

**6. David Beckham**

Mechi za Kombe la Dunia: 13

Ushiriki wa Kombe la Dunia: 1998, 2002, 2006

Jumla ya mechi za England: 115

Mchezaji pekee aliyeichezea England mechi 13 katika Kombe la Dunia, David Beckham ndiye mchezaji pekee kwenye orodha hii aliyetolewa nje kwa kadi nyekundu kwenye michuano hiyo.

**5. Bobby Moore**

Mechi za Kombe la Dunia: 14

Ushiriki wa Kombe la Dunia: 1962, 1966, 1970

Jumla ya mechi za England: 108

4. Ashley Cole

Mechi za Kombe la Dunia: 14

Ushiriki wa Kombe la Dunia: 2002, 2006, 2010

Jumla ya mechi za England : 107

England hawakubarikiwa haswa na safu ya mabeki wa kushoto katika miaka ya 2000, lakini walikuwa na mmoja wa wachezaji wa daraja la kimataifa katika nafasi hiyo duniani kupitia, Ashley Cole.

**3. Terry Butcher**

Mechi za Kombe la Dunia: 14

Ushiriki wa Kombe la Dunia: 1982, 1986, 1990

Jumla ya mechi za England : 77

Ingizo la kushangaza sana ukizingatia kwamba Terry Butcher alicheza mechi ya pili kwa England kwenye orodha hii, lakini mwanamume huyo alikuwa mshiriki mkuu wa timu za England miaka ya 1980 na mapema miaka ya 1990.

**2. Sir Bobby Charlton**

Mechi za Kombe la Dunia: 14

Ushiriki wa Kombe la Dunia: 1958, 1962, 1966, 1970

Jumla ya mechi za England: 106

Ushiriki wa Kombe la Dunia mara nne, Sir Bobby Charlton? Nne? Huo ni mwendawazimu.

Gwiji huyo wa Manchester United hakucheza mwaka wa 1958, lakini uteuzi wake katika kikosi cha Walter Winterbottom ulikuja miezi michache tu baada ya maafa ya ndege ya Munich.

**1. Peter Shilton**

Mechi za Kombe la Dunia: 17

Ushiriki wa Kombe la Dunia: 1982, 1986, 1990

Jumla ya mechi za England: 125

Mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi katika historia ya England. Mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi kwenye Kombe la Dunia. Hakika, Peter Shilton sasa anatumia siku zake kuingia kwenye mabishano kwenye Twitter, lakini bila shaka yeye ni mmoja wa wanasoka mahiri nchini humo.

## ISIKUPITE

KIUNGO wa zamani wa Arsenal na Timu ya Taifa ya England, Jack Wilshere ametangaza kustaafu kucheza soka akiwa na umri wa miaka 30. Wilshere ambaye maisha yake ya soka yamekwamishwa kwa kiasi na majeraha ni mhitimu wa shule ya vipaji ya Arsenal aliyeitumikia klabu hiyo hadi mwaka 2018 kabla ya kutimkia West Ham United.





# NAMNA STERLING ATAKAVYOFITI CHELSEA

**MANCHESTER, England**

RAHEEM Sterling atakuwa mchezaji wa pili msimu huu kuondoka Manchester City na kujiunga na mojawapo ya timu kuu sita katika ligi ya England baada ya kufikia makubaliano ya kibinafsi na Chelsea.

Baada ya kumuuza Gabriel Jesus kwenda Arsenal na kumsajili Halaand kutoka Borrusia Dortmund, City itakuwa tofauti katika safu ya mbele.

Chelsea pia itakuwa na mwonekano mpya, huku mshambuliaji wa England, Sterling akijiunga na miamba hiyo baada ya Romelu Lukaku kurudi Inter Milan.

Hivyo basi tunauliza Sterling ameacha nini City, kwanini anaondoka na ni nini atapeleka Chelsea?

City wameshinda mataji 29 makubwa katika historia yao, 12 kati ya hayo Sterling akiwa huko - ikiwa ni pamoja na mataji manne kati ya manane ya ligi, matano kati ya nane ya Kombe la Ligi na moja la Kombe la FA.

Anaondoka akiwa na mabao 131 na asisti 74 katika mechi 339 katika misimu saba baada ya kuhama kutoka Liverpool.

Pia amekuwa sehemu muhimu sana ya uongozi wa Pep Guardiola, akimchezea mechi (292) akiwa na mechi nyingi zaidi kwa raia huyo wa Katalunya kuliko mtu mwingine yeyote ndani ya klabu hiyo.

Ni Lionel Messi pekee (211) na Sergio Aguero (124) ambao wamefunga mabao mengi zaidi wakimchezea Guardiola kuliko 120 ya Sterling. Pia ni wa tatu kwa asisti, akiwa na 66, nyuma ya Kevin de Bruyne (105) na Messi (80).

"Amekuwa mchezaji muhimu sana katika misimu hii yote, mwenye mabao na pasi za mabao, na anapojiamini ni mchezaji muhimu sana," alisema Guardiola msimu uliopita.

Lakini pamoja na hayo, Sterling hajawahi kujionyesha kama gwiji machoni mwa mashabiki wa City.

"Sterling hajawahi kuwa kipenzi cha watu wengi, jambo ambalo ni gumu kulielezea kwani kwa sasa ameshinda mataji mengi ya Ligi Kuu ya England kuliko mchezaji yeyote asiye wa Manchester United isipokuwa John Terry na Fernandinho," alisema Simon Stone wa BBC Sport.

"Ubora wake umekuwa wa kusuasua. Wakati mwingine anaonekana kuwa mzuri sana, mara nyingine anaweza kupotea kabisa na bado anakosa nafasi mbele ya lango. Hata hivyo anabaki kuwa hatari akiwa na mpira miguuni mwake na siku zake bora bado zinaweza kuwa mbele.

"Anaweza kuwa mmoja wa wachezaji ambao wakati wao katika City unathaminiwa zaidi katika kumbukumbu kuliko ilivyokuwa wakati huo."

Kiwango kikubwa cha mafanikio ya Sterling katika City kinazua swali la wazi - kwa nini wanamruhusu kuondoka na kujiunga na mpinzani anayewahi kutoa ushindani mkubwa?

Kuna mambo mawili makubwa. Moja ni ukweli kwamba mkataba wake unakamilika msimu ujao kwa hiyo hii ilikuwa nafasi ya mwisho ya kujipatia fedha - jambo jingine ni usajili wa Haaland.

City mara nyingi wamecheza bila mshambuliaji halisi katika misimu michache iliyopita huku Aguero akijeruhiwa, na kisha kujiunga na Barcelona.

Lakini usajili wa pauni milioni 51 wa mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Haaland, ambaye amefunga zaidi ya mabao 150 akiwa na umri wa miaka 21, hakika utabadilisha yote hayo.

Ni mechi tisa tu kati ya 47 za Sterling msimu uliopita ambazo zilikuwa kwenye safu ya kati, lakini Phil Foden - ambaye alikuwa mshambuliaji wa kati mara 19 - alichukua nafasi ya winga muda mwingi.

Sterling alianzishwa mechi 23 pekee za Ligi Kuu msimu uliopita - na hiyo ilikuwa bila Haaland katika klabu hiyo.

"City haikutaka aondoke na ingefurahi kusalia kwake," aliongeza Stone. "Lakini alitaka kuwa sehemu muhimu ya timu inayoshindana katika kiwango cha juu. Pep kamwe asingeweza kuhakikisha hilo.

"Kwa kweli, wangeuzwa kwa klabu isiyo ya Ligi Kuu. Hata hivyo, kama Chelsea wangekuwa tayari kulipa zaidi ya mtu mwingine yeyote kwa mchezaji ambaye angeweza kuondoka bure katika muda wa miezi 12, kifedha, ni jambo la maana."

Kitu kimoja ambacho Chelsea watakuwa wakipata ni mabao na pasi za mabao, kitu ambacho wamekikosa licha ya mafanikio waliyopata hivi karibuni.

Mara ya mwisho kwa mchezaji wa Chelsea kufunga mabao mengi zaidi katika msimu mmoja kuliko Sterling - katika ligi na katika mashindano yote - alikuwa Diego Costa mnamo 2016-17.

"Kutokana na uwezo wake wa kufunga mabao, Sterling anaweza kuonekana kuwa bora zaidi kwa wale ambao tayari wapo na kufidia upungufu ulioachwa na Lukaku," alisema mtangazaji wa BBC Sport, Alistair Magowan.

"Pia anawakilisha taarifa ya nia kutoka kwa wamiliki wapya, ambao wanaelewe-ka kuwa na mipango kabambe katika soko la uhamisho.

"La muhimu zaidi, ni usajili wa kwanza kufanywa na Tuchel tangu apewe mamlaka zaidi chini ya mmiliki mwenza na mkurugenzi wa muda wa michezo, Todd Boehly kufuatia kuondoka kwa mshauri wa kiufundi na utendaji Petr Cech na Mkurugenzi Marina Granovskaia, ambao walishughulikia mazungumzo."

Tangu 2017-18, mshambuliaji huyo wa England amefunga mabao 110 na kutengeneza mengine 51 katika mashindano yote akiwa na City.

Olivier Giroud (39) - sasa yuko AC Milan - na Eden Hazard (38) wanasalia kuwa wafungaji bora wa Chelsea katika muda huo. Hazard aliondoka kwenda Real Madrid miaka mitatu iliyopita. Willian, aliyeondoka miaka miwili iliyopita, ndiye msaidizi wao bora akiwa na 31.

Sterling anaweza kuingia kama namba tisa wa uongo, mfumo ambao kocha wa Chelsea Tuchel anaonekana kuupendelea. Kuna uwezekano mkubwa zaidi Chelsea kucheza bila mshambuliaji sahihi baada ya kumtuma mfungaji bora wa msimu uliopita Lukaku kwa mkopo kwenda Inter Milan.

Msimu uliopita Sterling aliangushwa mara nyingi zaidi kwenye eneo la kisanduku cha wapinzani (8.93) kwa dakika 90 kuliko mshambuliaji yeyote wa Chelsea ambaye amesalia kwenye klabu hiyo.

Pia alijaribu na kukamilisha chenga nyingi zaidi kuliko washambuliaji wowote wa Blues. Hakim Ziyech na Mason Mount walicheza pasi nyingi kuliko Sterling na licha ya kufunga mabao mengi - Sterling alipiga mashuti machache kuliko Ziyech, Timo Werner, Mount na Kai Havertz kwa dakika 90.

Chelsea tayari wana chaguo mbadala kwenye safu ya ushambuliaji, lakini wanahitaji mtu ambaye hutengeneza na kufunga mabao mara kwa mara.

"Kuwasili kwa Sterling kutasababisha maswali kuhusu mustakabali wa washambuliaji wa pembeni Werner, Christian Pulisic na Ziyech," alisema Magowan.

"Wote walisajiliwa kabla ya Tuchel kuteuliwa katikati ya msimu wa 2020-21.

"Pamoja na Sterling, shinikizo la ziada litakuwa kwa Tuchel. Kocha atahitaji magoli kurejeshwa, lakini mafanikio ya usajili yanaweza pia kutegemea Werner, Pulisic au Ziyech pia kuondoka kwenye klabu, ambayo itaepuka kuchanganyikiwa kwa muda wa kucheza na kusaidia kusawazisha vitabu vilivyo chini ya umiliki mkubwa wa hisa za kibinafsi."

## Nukuu

"ILIKUWA ndoto kwamba, nililazimika kushinda kombe Amerika Kusini. River ilipoondolewa, uwezekano huo umefifia. "Mwezi mmoja na nusu uliopita nilitamka kwamba, sitaondoka Ulaya, lakini River alisisitiza na kusisitiza sana kwamba, nilikuja kulitafakari na kulikuwa na uwezekano."
**Luis Suarez**



"SITOKUWA karibu tena na GSM mimi nitakuwa upande wa Yanga kama msimamizi wa klabu, sitohusika na mikataba ya GSM kwa Yanga." **Injinia Hersi Said rais wa Yanga**



"FRENKIE de Jong ni mchezaji wa Barca na anatambulika kama mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani. Tunajua klabu zinazomtaka, sio Manchester United pekee, na hatuna nia ya kumuuza." **Joan Laporta rais wa Barcelona.**



# MAKOCHA 11 WAVYOTIMULIWA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara ilimalizika Juni 29, huku makocha 11 wakitimuliwa mpaka ligi hiyo ilipomalizika.

Makocha hao wa ndani na nje ya nchi walionyeshewa milango ya kutokea na klabu zao wakati ligi inaendelea kwa sababu za kufanya vibaya kwenye ligi hiyo iliyokuwa na mshikemshike wa aina yake, ilioanza kutimua vumbi Septemba 27, mwaka jana.

Hata hivyo, kuna mzunguko fulani wa kufurahisha, kwani baadhi ya makocha walikuwa wakitimuliwa huku na kuchukuliwa kwingine.

Anayetimuliwa timu moja, anakwenda kwenye timu ambayo nayo imetimua kocha.

Rekodi inaonyesha kuwa makocha 11 waliotimuliwa, saba ni wa kigeni na watatu ni wazawa.

Kwenye makala hii, mwandishi ameorodhesha makocha wote ambao Ligi Kuu Tanzania Bara ilikuwa ngumu kwao na wakatimuliwa, kabla haijamalizika.

**1. Etienne Ndayiragije-Geita Gold**

Kocha huyu wa zamani wa klabu za Mbao FC, Azam FC na timu ya taifa, Taifa Stars alichukuliwa na Geita Gold iliyopanda na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu huu, Agosti mwaka jana.

Alipewa jukumu la kuinoa timu hiyo akitarajiwa kufanya makubwa. Katika hali isiyokuwa ya kawaida, Mrundi huyu alitimuliwa kazi miezi miwili baadaye, kisa timu haifanyi vizuri. Kocha Msaidizi Fred Felix Minziro akachukua jukumu.

Na kweli akaibadilisha timu na ikamaliza Ligi Kuu ikiwa kwenye nafasi ya nne, ikipata nafasi ya kucheza Kombe la Shirikisho Afrika kwa mara ya kwanza kwenye historia yao.

**2. Didier Gomes-Simba**

Aliondoka kwenye klabu ya Simba Oktoba mwaka jana, baada ya kushindwa kuipeleka timu hiyo kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Didier Gomes, raia wa Ufaransa, alijiunga na Simba mwanzoni mwa mwaka huu akitokea Al Merrikh ya Sudan. 'Alitimuliwa kiaina', baada ya Simba kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa.

Pia Simba ilionekana haichezi vizuri kwenye Ligi Kuu na kutopata matokeo ya kuridhisha sana,

Hata kabla ya ushindi, haukuonekana kuwafurahisha wanachama na mashabiki wa Simba kutokana na mfumo na aina ya uchezaji wa wachezaji wake, hivyo naye panga likampitia.



Ettiene Ndayiragije, raia wa Burundi, mmoja wa makocha 11 walioonyeshwa mlango wa kutokea na timu zao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/22.

**3. Haruna Hererimana-Mbeya Kwanza**

Klabu ya Mbeya Kwanza ilimtimua kocha wake Haruna Hererimana raia wa Burundi kwa madai ya timu kupata matokeo mabovu kwenye mechi za Ligi Kuu, ikimchukua kocha wa zamani wa Mbeya City, Maka Mwalwisi. Alichukua timu Agosti mwaka jana, lakini timu ilipofanya vibaya, viongozi hawakusubiri. Haikuwa dawa, kwani pamoja na kubadilisha kocha, mara ya mwisho ikiwa na Mbwana Makata ambaye akaja kufungiwa, Mbeya Kwanza ilikuwa timu ya kwanza kuteremka daraja msimu huu.

**4. George Lwandamina-Azam FC**

Kocha huyu mkongwe raia wa Zambia, alitimuliwa katikati ya mwezi Desemba mwaka jana baada ya shinikizo kubwa kutoka kwa mashabiki wa Azam FC.

Lwandamina, kocha wa zamani wa Yanga, alipewa kibarua hicho Desemba mwanzoni mwaka jana,

lakini baada ya kuona kila kukicha afadhali ya jana, uongozi wa Azam ukaamua akae pembeni.

**5. James Omog-Mtibwa Sugar**

Alitimuliwa katikati ya Desemba mwaka jana baada ya jahazi la Mtibwa Sugar kuonekana kuzama siku hadi siku. James Omog, raia wa Cameroon, kocha wa zamani wa Azam FC na Simba, aliletwa nchini ikionekana kama itakuwa suluhisho la kuboronga na Mtibwa Sugar msimu uliopita, lakini ikawa afadhali hata ya msimu uliopita kuliko huu. Ikamchukua Mayanga ambaye alikuwa ametimuliwa na Prisons. Angalau timu ikaanza kufanya vema, na hivi majuzi aliiongoza Mtibwa kwenye mechi za mchujo dhidi ya timu yake ya zamani iliyomtimua, akafanikiwa kuibakisha Ligi Kuu.

**6. Hemed Morocco-Namungo**

Baada ya misimu miwili ya mafanikio, hatimaye Hemed Morocco akaondoka kwenye klabu ya Namungo.

Ilikuwa ni Desemba mwaka jana alipoondoka baada ya timu kutofanya vema kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Klabu hiyo ikamtwaa Kocha raia wa Zambia, Hanoor Janza na msaidizi wake Jamhuri Kihwelo ambao, angalau ikamaliza Ligi Kuu kwenye nafasi ya tano.

**7. Patrick Odhiambo-Biashara United**

Mkenya huyu ambaye kwa sasa anaifundisha Prisons, inayohangaika kwenye 'play off'' ya pili, baada ya kugongwa ya kwanza dhidi ya Mtibwa Sugar.

Alikuwa kocha mwingine wa kigeni kutimuliwa kwenye Ligi Kuu. Yeye alitimuliwa na klabu ya Biashara United baada ya timu hiyo kuboronga, na nafasi yake ikachukuliwa na Vivier Bahati aliyekuwa kocha msaidizi wa Azam FC, ambaye alitimuliwa pamoja na George Lwandamina. Bahati naye hakukaa. Mwishoni ilikuwa inafundishwa na Khalid Adam kabla ya kuwa timu ya pili kushuka daraja.

**8. Vivier Bahati-Biashara United**

Mrundi huyu anaweka rekodi ya kuwa kocha aliyetimuliwa mara mbili kwenye klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika.

Akiwa Kocha Msaidizi wa Azam alitimuliwa na Kocha Mkuu Lwandamina kwenye klabu ya Azam FC, akaenda kuwa Kocha Mkuu wa Biashara United. Hata hivyo hakufanya kile ambacho waliomchukua walikitegemea na timu ilizidi kupoteza mechi wiki hadi wiki, naye akatimuliwa, nafasi yake ikachukuliwa na Khalid Adam ambaye aliishusha kabisa.

Biashara United nayo inaingia kwenye rekodi ya kutimuwa makocha mara mbili kwenye Ligi Kuu, Odhiambo na Vivier, ambapo hata hivyo haikuwasaidia kuepuka kaburi la kushuka daraja.

**9. Salum Mayanga-Prisons**

Alikuwa ni kocha wa Prisons. Naye alitimuliwa baada ya timu kuonekana haifanyi vema na badala yake, akaletwa kocha Patrick Odhiambo ambaye naye alitoka kutimuliwa kwenye klabu ya Biashara United.

Mayanga akachukuliwa na Mtibwa Sugar akichukua mikoba ya Omog na kufanikiwa kuibakisha timu hiyo Ligi Kuu kwenye mechi ya mchujo dhidi ya timu iliyomtimua, Prisons.

**10. Mbwana Makata-Dodoma Jiji**

Kutokana na mlolongo wa matokeo yasiyoridhisha, hatimaye viongozi wa Dodoma Jiji, wakatangaza kumtupia virago kocha Mbwana Makata, ambaye aliipandisha daraja.

Klabu hiyo ikamchukua Kocha Msaidizi wa zamani wa Simba, Masoud Djuma, ambaye hadi leo ndiye anayekinoa kikosi hicho.

Makata yeye baada ya kutimuliwa alichukuliwa na Mbeya Kwanza, ikampata balaa ya kufungiwa kutokana na utovu wa nidhamu.

11. Melis Medo-Coastal Union

Kocha huyo raia wa Marekani alianza kwa mbwembwe kubwa kwenye kikosi cha Coastal Union, lakini kadri muda ulivyozidi kusonga mbele hali ilikuwa mbaya.

Ilifika wakati Coastal Union ikawa haijashinda mechi yoyote kwa mwezi mzima.

Viongozi wa Coastal Union wakafanya maamuzi magumu ya kumtimua. Waliwashangaza wengi walipomrudisha Juma Mgunda ambaye kwa muda mrefu alikuwa amebadilishiwa majukumu na kuwa Mkurugenzi wa Ufundi badala ya kocha.

Maamuzi hayo yalilipa, kwani Coastal si tu kwamba ilitoka kwenye tishio la kushuka daraja, bali ilifika fainali ya Kombe la FA na ikatolewa kishujaa.

**JE, WAJUA?**



MASHABIKI wa soka watalazimika kuzoea maisha bila kutumia kilevi baada matumizi ya pombe ndani ya viwanja nchini Qatar kupigwa marufuku wakati wa michuano ya Kombe la Dunia.





# Kamati Bunge yaridhishwa ujenzi miundombinu fedha za UVIKO-19

**Na Mwandishi Wetu,** KONDOA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imeridhishwa na ujenzi wa miundombinu inayojengwa kupitia fedha za Mradi wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19, katika Pori la Akiba Mkungunero, mikoa ya Dodoma na Manyara kuvutia watalii.

Akizungumza katika ziara ya kamati hiyo mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa Kamati, Daniel Sillo, alisema miradi hiyo inatekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), katika fedha hizo ilipewa Sh. bilioni 12.9 huku Pori la Akiba la Mkungunero likipatiwa Sh. milioni 672.

Alisema ameridhishwa na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa lango la kuingilia wageni, barabara ya kilomita 47.2 na ujenzi wa 'Picnic Site' kwenye pori hilo.

"Spika wa Bunge aliridhia Kamati ya Bajeti kupitisha Sh. trilioni 1.3 Mradi wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 ambapo kati ya hizo Wizara ya Maliasili na Utalii ilipewa Sh. bilioni 90.2."

Alisema sekta ya utalii inachangia asilimia 17 ya Pato la Taifa na asilimia 25 ya pato la kigeni, anaamini kwa siku za mbele uchangiaji utaongezeka zaidi.

"Niwashauri endeleeni kusimamia miradi hii niwaombe msimamie vizuri miradi hii ili iweze kuleta tija," alisema.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema katika fedha za UVIKO-19, TAWA inatekeleza miradi mbalimbali kwenye maeneo inayosimamia ili kuwa na miundombinu inayovutia watalii.

Awali, Kaimu Naibu Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA, Mlage Kabange, alisema pori hilo lina ukubwa wa kilomita za mraba 743 na ni miongoni mwa mapori 27 yanayosimamiwa na TAWA.

Alisema asilimia 92 ya eneo la pori hilo lipo Dodoma katika Wilaya ya Kondoa na asilimia nane ipo katika Wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara likiwa na faida za kiikolojia na makazi ya wanyama mbalimbali wakiwamo tembo na tandala.

"Hapa kuna simba, chui na kuna nyuki na kuna mambo mazuri sana ikiwamo ya kiikolojia ambayo inasababisha baadhi ya maeneo hasa vijiji vya jirani kuweza kupata maji," alisema.

Kadhalika, kuna fursa za utalii zinazopatikana kupitia pori hilo na watu mbalimbali kufika kuwinda na pia ni dakio la maji katika Mto Tarangire.



Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu (wapili kushoto), akizungumza na wajane na yatima wakati wakisubiri kupatiwa sadaka kwa ajili ya sikukuu ya Eid El- Hajj, iliyoandaliwa na Msikiti Mkuu wa Gadafi, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC ashauri wamiliki nyumba, shule kufunga kamera CCTV

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUTOKANA na kuibuka kwa matukio mengi ya wizi katika Jiji la Dodoma, Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka amewataka wamiliki wa nyumba na shule kufunga mifumo ya kamera za ulinzi (CCTV).

Mtaka alibainisha hayo juzi wakati alipotembelea Shule ya Sekondari Miyuji ya jijini hapo kuona jinsi ilivyofanikiwa kudhibiti matukio ya wizi na utoro kwa walimu na wanafunzi wakati wa masomo.

Alisema kutokana na matukio ya wizi yanayojitokeza jijini hapo, wamiliki wa nyumba hawana budi kufunga kamera hizo za ulinzi ili kudhibiti hali hiyo.

"Ni wakati sasa tukabadilika wamiliki wa nyumba kutokana na ongezeko la watu jijini Dodoma kumekuwapo na matukio mengi ya wizi hivyo kufunga kamera kunaweza kuwa msaada kwetu kulinda mali zetu."

"Haiwezekani leo mtu anakuwa na uwezo wa kujenga nyumba ya milioni 30, lakini akashindwa kufunga mafumo wa kamera za ulinzi wa milioni mbili," alisema Mtaka.

Kadhalika, alizitaka shule za serikali Mkoa wa Dodoma kufunga kamera hizo ili kulinda mali pamoja na wanafunzi watoro wakati wa masomo.

"Nikupongeze sana mkuu wa shule hii kwa ubunifu huu wa kufunga kamera natumai utakuwa msaada mkubwa sana kwa shule kupunguza utoro wa walimu pamoja na wanafunzi wakati wa masomo," alisema.

Aliagiza kamati za taaluma za shule kufanya uchambuzi wa matokeo ya wanafunzi wa kidato cha nne, ili kuweka mikakati itakayo wasaidia kuondokana na matokeo mabaya kwenye mtihani wa mwisho.

"Maagizo yangu kamati zote za shule Mkoa wa Dodoma zihakikishe kuwa zinafanya uchambuzi ili kuona wanafunzi wote ambao walitoka kidato cha tatu kuja cha nne wenye daraja sifuri (Division zero), shule iweke mikakati ya kuwaondoa katika hatari hiyo ili kila mtoto atoke na cheti cha kidato cha nne katika mtihani wao unaotarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu," alisema.

Naye Mkuu wa shule hiyo, Greyson Maige, alisema mfumo wa kamera za ulinzi umewagharimu zaidi ya Shilingi milioni mbili na umesaidia kupunguza utoro kwa wanafunzi na walimu kuhudhuria kikamilifu katika vipindi vyao.

"Pia, tumeshabuni mfumo ambao utatumika kwa walimu kusaini wakati wa kuingia na kutoka kupitia simu zao za mkononi na mimi napata taarifa kupitia mfumo ambao pia umefungwa ofisini kwangu," alisema.

Hata hivyo, alisema shule hiyo inakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo uhaba wa matundu ya vyoo na idadi ndogo ya walimu wa

# Wazazi washauriwa umri kupeleka watoto vituoni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

VIONGOZI wa dini kwa kushirikiana na Mtandao wa Malezi na Makuzi ya Maendeleo ya Awali ya Mtoto (TECOAN), wametakiwa kutoa elimu ya malezi kwa jamii ili kupunguza kupeleka watoto wakiwa na umri mdogo kwenye vituo vya kulelea watoto (day care).

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ramadhan Kailima, alitoa kauli hiyo jana jijini hapo alipokuwa akifunga mafunzo ya wanahabari zaidi ya 70, yaliyoandaliwa Chuo Kikuu cha Aghakan, Shirika la Chidren Crossifire (CIC), wakishirikisha Muungano wa vilabu vya waandishi wa habari (UTPC).

Alisema elimu ya malezi na makuzi ni muhimu ikatolewa kwa jamii ili kuacha kukimbilia kupeleka watoto kwenye vituo hivyo wakiwa wadogo.

"Jamii imekuwa ikijisahau sana kwenye malezi ya watoto na kuwapeleka day care, hivyo haya mafunzo yatafutwe namna ya kuyaeneza katika maeneo mbalimbali ili kila mmoja aweze kutambua umuhimu wa malezi ya mtoto akiwa mdogo mpaka anakua," alisema.

Mkurugenzi CIC, Graig Ferla, alisema malezi na makuzi ya watoto ni muhimu kwa jamii ndiyo sababu iliyowasukuma kuandaa mafunzo hayo.

Ferla alisema anaamini washiriki ambao ni waandishi wa habari watakwenda kutumia kalamu zao kupaza sauti ili kuhakikisha elimu hiyo inawafikia jamii katika maeneo mbalimbali wanayotoka.

Tumekuwa tukifanya warsha ikiwamo kufanya tathmini kujua namna gani elimu ya malezi na makuzi imefikia jamii," alisema Ferla.

Mkurugenzi Mtendaji wa TECOAN, Mwajuma Rwebangila, aliishukuru serikali pamoja na wadau mbalimbali kwa kusaidia kuhakikisha sauti ya malezi ya mtoto inapazwa nchini.

Aliwataka waandishi wa habari kutumia kalamu zao ipasavyo, ili kusaidia kuielimisha jamii suala hilo na kuondokana na kero za malezi.





# Azindua zahanati iliyojengwa kwa nguvu za wananchi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MBUNGE wa Jimbo la Lupa, wilayani Chunya, Masache Kasaka, amezindua zahanati ya Kijiji cha Itumba iliyojengwa kwa nguvu za wananchi na serikali kwa gharama ya Sh. milioni 71.5 na kuwasisitiza wananchi kujiunga na bima ya afya iliyoboreshwa.

Kasaka alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipozungumza na wananchi wa Kijiji cha Itumba baada ya uzinduzi wa zahanati na kuwaeleza wananchi faida za bima ni kuwa na uhakika wa matibabu bila malipo.

Tumeshapata zahanati hapa ndugu zangu ugonjwa haupigi hodi nawahamasisha jiungeni na mfuko wa bima iliyoboreshwa (CHIF) ili muweze kutibiwa bila usumbufu pindi mnapofika kwenye zahanati yetu, kwa sababu huwezi kuwa na fedha muda wote," alisema Kasaka.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Dk. Dariso Andrew, alisema ujenzi huo ulianzishwa kwa nguvu za wananchi mwaka 2017 na serikali baada ya kuona juhudi za wananchi iliamua kuwaunga mkono hadi kituo hicho kukamilika.

Alisema wamepokea watumishi wapya wa kada ya afya na kinachoendelea kwa sasa ni kupangiwa maeneo yao ya kazi ikiwamo zahanati hiyo ambayo itapata wahudumu wa kutosha.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Itumba walisema zahanati hiyo itasaidia kupunguza adha waliyokuwa wakipata awali hasa wajawazito wakati wa kujifungua ambao awali walilazimika kwenda vijiji vya mbali kufuata matibabu.

# Mbeya yashindwa kufikia lengo ufaulu kidato VI

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umeshindwa kufikia malengo waliyojiwekea ya kufaulisha wanafunzi wa kidato cha sita kwa wastani wa GPA 2.5 mwaka huu na badala yake wameambulia kufaulisha kwa wastani wa GPA 2.9 na sababu za kushindwa kufikia lengo hilo.

Siku chache baada ya Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), kutangaza matokeo ya kidato cha sita, wadau wa elimu mkoani hapa wamekutana kufanya tathmini ya ufaulu wa mtihani huo. Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Ernest Hinju, alieleza hali ya ufaulu wa mkoa huo kuwa walijiwekea malengo ya kufikia wastani wa 2.5, lakini imekuwa tofauti.

Hata hivyo, alisema matokeo hayo sio mabaya na wamefanya tathmni na kujipanga kwa ajili ya mwaka ujao ambao wameahaidi kufanya vizuri zaidi ikilinganishwa na miaka iliyopita.

"Mwaka jana tulifanya vizuri sana tulifikia wastani wa 3.1 mwaka huu ndiyo hivyo tumepata chini ya hapo, kikao hiki kimetusaidia kuweka mikakati ya kufanya vizuri zaidi katika matokeo yajayo maana tumebaini tulichelewa kuweka mipango yetu kwenye utekelezaji," alisema Hinju.

Baadhi ya walimu na wakuu wa shule za sekondari mkoani hapo walieleza mikakati waliyonayo ya kufikia malengo ya ufaulu kwenye shule zao.

Ofisa Elimu Sekondari, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Aliko Mbuba, alisema suala la ufaulu ni mchakato hauwezi kupanga mipango kwa wakati mmoja na kutegemea matokeo haraka, wamelichukulia kwa uzito mkubwa na wanaendelea kujipanga na kufanya vizuri kwenye matokeo yajayo.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Mbeya Day, Francis Mwakihaba, alisema kwa sasa wameweka malengo katika kila somo ili mwalimu afikishe wastani kadhaa hali ambayo itasaidia kujituma.

Alisema utaratibu huo unatoa tathmini kwa mwalimu kujijua kafikisha wastani kadhaa kwenye somo lake ili kujua wapi anapaswa kuboresha.

Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, aliwaagiza wazazi, kushirikisha jamii kwenye maendeleo ya kitaaluma kwa mtoto kikamilifu.

Alisema kwa kufanya hivyo watashikamana na kuwa kitu kimoja na hatimaye kusaidia mkoa huo kufanya vizuri kwenye mitihani mbalimbali ya ndani ya mkoa na kitaifa.




Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. William Anangisye (wa pili kushoto) akikabidhi Ripoti ya Utafiti wa Gesi Ukaa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Simbagas, David Ndelwa, kwa ajili ya kampuni hiyo kuanza uchimbaji wa gesi hiyo, mkoani Mbeya, katika hafla ilifanyika UDSM mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera na (wa pili kulia kulia) ni Dk. Elisante Mshiu kutoka UDSM aliyefanya utafiti huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waomba viwanda kuongeza thamani zao la parachichi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

LICHA ya hali ya hewa kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuwa ya baridi kali na kusababisha upatikanaji wa mazao kama parachichi kutopatikana kwa wingi, wazalishaji wa miche ya matunda hayo mkoani hapo, wamewaomba wadau na serikali kujenga viwanda vya kuongezea thamani zao hilo ili kuwasaidia kupata soko la uhakika kwa wakulima wanapozalisha.

Ombi hilo lilitolewa jana na wanakikundi cha parachichi kwanza kilichoko jijini hapo kinachojishughulisha na uzalishaji miche ya zao hilo.

Miongoni mwa wakulima, Janeth Mwamlima, alisema shughuli hiyo imewasaidia kumudu gharama za maisha kwa kila mmoja wao na uwapo wa viwanda vya kutengeneza mafuta ya kupakaa yatokanayo na parachichi utasaidia kuongeza mahitaji ya zao hilo sokoni na wazalishaji kufaidika.

Alisema kuongezeka kwa mnyororo wa thamani wa zao hilo itakuwa na manufaa makubwa kwa sababu mahitaji ya miche yatakuwa makubwa na kuongeza kiwango cha kuzalisha. James Pilla, alisema kuwa licha ya kuanzisha kikundi cha parachichi kwanza mwaka 2021 na kutambuliwa na Serikali ya Mkoa wa Mbeya, wameanza kupata tenda mbalimbali kutoka kwa kampuni na wakulima wakihitaji miche ya kupanda.

Alisema licha ya kuanzisha kikundi hicho, hawana maarifa ya kutosha kuhusu uzalishaji wa miche ya matunda hayo na kuomba Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania Tari, Kituo cha Uyole kuwapatia elimu ya kuzalisha kwa kuzingatia ubora.

"Baada ya kuanzisha kikundi chetu cha kuzalisha miche bado tulikuwa tunashindwa kuzalisha katika ubora unaotakiwa hivyo sisi waoteshaji tuliwaomba wataalamu wa kilimo kutoka Tari Uyole watupatie elimu ya kuandaa vitalu na kuotesha miche kwa kuzingatia kanuni za kilimo bora," alisema Pilla.

"Tuliamua kutembelea kituo cha Utafiti wa Kilimo Tanzania Tari, Uyole kwa lengo la kujifunza njia za kisasa za kuzalisha miche bora ya parachichi ukizingatia zao hili ni la kimkakati tumefundishwa mambo mengi ambayo yatasaidia kuzalisha kwa tija," aliongeza Pilla.

Alisema zao hilo ni fursa kwa sababu limetoa ajira kuanzia wazalishaji wa miche na wakulima shambani pamoja na wanunuzi, wazalishaji wamejipanga vizuri kuongeza ujuzi wa namna bora ya kuzalisha miche ambayo itatoa matunda mazuri yatakayoweza kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

"Ni fursa kwa Mkoa wa Mbeya na nje ya nchi kulima zao la parachichi ambalo kwa sasa limekuwa dhahabu ya shambani sisi waoteshaji wa vitalu vya miche tunaendelea kuongeza maarifa ya namna bora ya kuazalisha miche ambayo itazalisha matunda yanayohitajika katika soko la kimataifa," alisema Pilla.

Alisema soko la miche linazidi kukua kila siku na kabla ya kujiunga kwenye kikundi hicho alikuwa na uwezo wa kuzalisha miche 5000 hadi 7000 kulingana na mahitaji ya soko la dunia.

Alisema katika kikundi chao wanatarajia kuandaa kitalu na miche kati ya 20,000 hadi 30,000 kwa mwaka 2022/2023.

Mtafiti wa zao la parachichi kutoka Kituo cha Utafiti wa Kilimo Tari Uyole, Daud Mbongo, alisema waliamua kukisaidia kikundi hicho kuwapatia elimu ya uzalishaji bora wa miche ili waweze kuzalisha kwa tija na kupata soko la ndani na nje ya nchi.

Alisema walifikia uamuzi wa kukisaidia kikundi hicho baada ya kubaini upungufu katika uzalishaji wa miche hiyo na walianzisha darasa la kuwafundisha mbinu mbalimbali za kuwawezesha kuzalisha kwa kuzingatia ubora unaotakiwa.

Tunaamini kwamba tukimpatia elimu huyu mzalishaji wa miche atawasaidia wakulima na watafika katika eneo lake la kazi atamweleza namna bora ya kulima zao hilo na kupata mavuno mengi.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania, Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema kituo hicho kinafanya utafiti wa mazao mbalimbali ikiwamo matunda. Alisema ubora wa zao la parachichi unahitajika kuanzia maandalizi ya kulima hadi kuvuna ili kupata soko la uhakika ndani na nje ya nchi wakaomba wadau wawasaidie wakulima kuwapatia elimu ya uzalishaji bora na mafunzo.







Mshauri wa Rais wa Zanzibar masuala ya Siasa, Ali Salum Haji (Kirova), akizungumza wakati akitoa salamu za mkono wa Idd El Hajj kwa niaba ya mke wa Rais Mama Mariam Mwinyi, kwa wazee wa Nyumba za Wazee Sebleni na Welezo, Mjini Magharibi jana, ikiwa ni utaratibu wa mke wa Rais kila ifikapo kipindi cha sikukuu. **PICHA: IKULU**

# Wasaidizi wa sheria watakiwa kusaidia jamii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka wasaidizi wa sheria kuendelea kuhamasisha jamii katika masuala mbalimbali ya kisheria ili kupunguza matendo maovu nchini.

Hemed aliyasema hayo jana katika maadhimisho ya tatu ya wiki ya msaada wa kisheria mjini hapo yaliyofanyika Kikwajuni.

Alisema juhudi zinazochukuliwa na wasaidizi hao ni za kupongezwa na kuwataka wasaidizi hao kuongeza kasi mijini na vijijini kwa kuhamasisha uwapo wa sheria hasa utoaji wa ushahidi kwenye kesi za udhalilishaji.

Kadhalika, alisema jamii inakumbwa na tatizo la uelewa mdogo wa utoaji wa ushahidi hasa vijijini katika kesi za udhalilishaji na kwamba kufika kwao kwenye maeneo hayo kutasaidia.

Aliziagiza mamlaka zinazosimamia ushahidi kuhakikisha wananchi hawapati usumbufu wa aina yoyote wanapoitwa kwa kutoa ushahidi hasa ikizingatiwa baadhi hukaa muda mrefu bila ya mafanikio.

Alisema, serikali haifurahishwi kuona kesi zinachelewa kukamilika kwa kisingizio cha kutokamilika kwa upelelezi na kuzitaka mamlaka husika kusimamia upelelezi wa kesi ili zikamilike kwa wakati na kuzingatia haki.

"Kuendelea kuwa na mrundikano wa kesi ambazo zinaelezwa kuwa upelelezi haujakamilika hili halina tija na halileti sura nzuri kwa nchi," alisema.

Hemed aliwasisitiza wanasheria kusimamia haki nchini ili wananchi wawe na imani na serikali yao ikiwa ni miongoni mwa ahadi za Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kipindi akiomba ridhaa za Wazanzibar.

Hata hivyo, alisema kutokuwapo suala la utoaji haki kunasababisha kuchelewa kwa maendeleo nchini.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Harun Ali Suleiman, ameutaka uongozi wa Shule ya Sheria Zanzibar, kuandaa mafunzo kwa wasaidizi wa sheria kwa kushirikiana na Shirika la Msaada wa Kisheria (LSF) ili kuongeza ujuzi kwa wasaidizi hao na kufanyakazi vizuri na kujiamini.

Waziri Harun alisema kesi za udhalilishaji zinakithiri kila siku na kuwa jamii inahitaji nguvu za ziada ili kuongeza uelewa kwa jamii na kusimamia haki.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria, Hanifa Ramadhan Said, alieleza kuwa wiki ya msaada wa kisheria ni muda muafaka kwa wasaidizi wa kisheria kukaa pamoja na taasisi mbalimbali kujitathmini kujua namna walivyofanikiwa katika kuisaidia jamii.

Mwakilishi wa watoaji msaada wa kisheria, Shaban Sarboko, ameishukuru Serikali ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa kuendelea kuwaunga mkono katika harakati zao za kuitumikia jamii.

Alisema kuwa licha ya uwajibikaji wao bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ukosefu wa rasilimali watu, vifaa pamoja na ofisi ambazo zinasababisha kuwa kikwazo katika kazi zao za kila siku.

# Jamii yaaswa uovu, uhujumu uchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, ameitaka jamii kutoficha uovu wowote unaotokea kwenye vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi hasa katika miradi inayotekelezwa na fedha za ahuweni za UVIKO-19.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mapambano dhidi ya Rushwa Afrika katika mkutano uliofanyika ofisini kwake.

Alisema jukumu la kuzuia na kupambana na rushwa sio la mamlaka pekee bali linajumuisha wananchi katika ngazi zote, juhudi zinahitajika kutoka kwa wadau mbalimbali wa mapambano dhidi ya rushwa ili kuhakikisha rushwa inapungua na kumalizika kabisa.

Alisema Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), imefuatilia miradi ya fedha hizo za ahueni inayotekelezwa na taasisi mbalimbali na imepata mafanikio kwa kiasi kikubwa licha ya kuwapo changamoto ndogo.

"Ili kufikia lengo hilo ni jukumu la kila mwananchi kuhakikisha uovu na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi hasa katika miradi inayotekelezwa kwa fedha za ahueni za UVIKO-19 vinatolewa taarifa ili hatua za kisheria kuchukuliwa kwa wahusika," alisema Waziri Haroun.

Aidha, alisema mamlaka inaendelea kufanya jitihada za udhibiti ili kubaini mianya inayotumiwa na watu wasiokuwa waaminifu katika taasisi za umma na binafsi kuhakikisha vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi wanavitokomeza nchini.

Alisema rushwa ni tatizo kubwa hasa kwa jamii ya Afrika kwa sababu hudumaza maendeleo na kuchochea umaskini hali inayosababisha watu kukosa huduma za lazima, ikiwa Zanzibar ni sehemu ya Afrika inaungana na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika kuadhimisha siku hiyo.

Maadhimisho hayo hufanyika kila Julai 12 na kwa upande wa Zanzibar ikiwa Umoja wa Afrika utaadhimisha siku hiyo leo.

# Waziri aiagiza ZAWA kutafuta mashine kusukuma maji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Shaibu Hassan Kaduara, ameiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Maji Zanzibar (ZAWA), kutafuta mashine ya kusukumia maji.

Alisema ni lazima mashine hiyo ipatikane haraka ili wananchi wa Kizimkazi Mkunguni waendelee kupata huduma ya majisafi na salama.

Aliyasema hayo wakati alipofanya ziara ya kutembelea kianzio cha maji katika kijiji cha Kizimkazi kutokana na wananchi wa eneo hilo kukabiliwa na tatizo hilo.

Alifafanua kuwa maelekezo hayo ZAWA ina uwezo wa kununua mashine na wananchi wakapata maji.

"Kama utakumbuka kesi kama hii iliwahi kutokea Jambiani, ZAWA ni mamlaka ya serikali wanajua wapi watapata mashine ya maji, na Serikali ya Zanzibar haishindi kuwaletea wananchi huduma ya maji kwasababu ya mashine moja kuharibika," alisema.

Aliiagiza ZAWA kununua mashine mbili za maji zenye uwezo wa ukubwa wa ujazo wa kilowati 11 ili wananchi wa maeneo hayo waendelee kupata huduma hiyo.

Alisema tatizo la maji litakwisha baada ya kumalizika mradi mkubwa wa maji ambao unategemewa kuwa na tangi la lita milioni tano kwa mujibu wa wataalamu.

Alisema mradi huo upo katika hatua ya awali na unadhamiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, lakini akitokea mfadhili serikali itampokea lengo kuu ni hufikisha huduma kwa wananchi wote wa Zanzibar waondokane na usumbufu wa kutafuta maji.

Naye Mkurugenzi Rasilimali Maji kutoka ZAWA, Maulidi Hassan Khamis, alisema tatizo la ukosefu wa maji linatokana na kuungua mashine moja ya kusukumia.

Pia, alisema mashine iliyoko uwezo wake ni mdogo kilowati 9.2 na kusababisha kutoa maji kwa mgawo ili kuipumzisha.

Kwa upande wake Farida Mohamed Khamis, mkazi wa kijiji hicho, alisema wanapata maji kwa mgawo kila baada ya siku mbili jambo ambalo halikidhi mahitaji kutokana na umuhimu wa huduma hiyo.

HABARI PICHANI

# SHEREHE ZA EID EL HAJJ



Rais Samia Suluhu Hassan akitoka katika swala ya Eid El- Hajj, kwenye Msikiti maarufu 'Msikiti wa Mwinyi', Mikocheni B, Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**



Sehemu ya waumini wa dini ya kiislamu wakiswali swala ya Eid El Hajj, katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi (wa tatu kulia), akifuatilia hotuba ya Baraza la Eid El Hajj, katika ukumbi wa Chuo cha Amali Mkokotoni, Mkoa wa Kaskazini Unguja jana. Kulia kwake ni Mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Mama Zainab Kombo Shaib na Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma na (kushoto kwake) Mke wa Makamu wa Pili wa Rais, Mama Sharifa Omar Khalfan na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Mhandisi Zena Ahmed Said. **PICHA: IKULU**



Baadhi ya wananchi wakichinja wanyama ikiwa ni sehemu ya kutekeleza ibada ya Eid El Hajj, iliyoswaliwa jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Sheikh Yahaya Abubakari, akitoa hotuba baada ya swala ya Eid El Hajj, katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Ofisa Kitengo cha Mawasiliano katika Ofisi ya Rais Zanzibar Ikulu, Khadija Pembe Juma (kushoto), akitoa mkono wa Idd El Hajj, kwa wazee wanaoishi nyumba za wazee Sebleni, Zanzibar jana, kwa niaba ya Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi, ambapo ni utaratibu wake kila ifikapo kipindi cha sikukuu. **PICHA: IKULU**

HABARI KIMATAIFA

# Rais, Waziri Mkuu Sri Lanka wajiuzulu

**COLOMBO, Sri Lanka**

RAIS wa Sri Lanka, Gotabaya Rajapaks na Waziri Mkuu, wamekubali kujiuzulu baada ya kutokea kwa maandamano na wananchi kuyateka majengo ya Ikulu.

Maandamano hayo yaliyoambatana na vurugu zilizosababishwa na nchi hiyo kutumbukia kwenye mzozo mkubwa wa uchumi.

Waandamanaji walivamia makazi ya viongozi hao wawili na kuchoma moto ofisi ya waziri mkuu kwa hasira.

Waziri Mkuu, Ranil Wickremesinghe, alisema ataachia ngazi baada ya serikali mpya kuingia madarakani, na saa chache baadaye spika wa bunge alitangaza Rais Rajapaksa amekubali kujiuzulu pia.

Shinikizo lilizidi kuongezeka kwa viongozi hao wawili baada ya mdororo wa kiuchumi kusababisha uhaba mkubwa wa bidhaa muhimu, na kusababisha watu wakihangaika kununua chakula, mafuta na mahitaji mengine.

Polisi Sri Lanka ilijaribu kuzuia maandamano hayo kwa kutoa amri ya watu kutotoka nje na baadaye kuiondoa amri hiyo baada ya wanasheria na wanasiasa wa upinzani kuikosoa amri hiyo na kuitaja kuwa kinyume cha sheria.

Maelfu ya waandamanaji walimiminika katika mji mkuu Colombo na kuyavamia makazi ya Rajapaksa.

Baadhi ya picha za video zimeonyesha umati mkubwa wa watu wakisherehekea ndani ya kidimbwi cha kuogelea, huku wengine wakilala kwenye vitanda na kujipiga picha ndani ya majengo ya Ikulu.

Baadhi ya watu walipika chai, huku wengine wakitoa tangazo kutoka chumba cha mikutano wakiwataka rais na waziri mkuu kuondoka.

Haikuwa wazi iwapo Rajapaksa mwenyewe alikuwapo wakati huo, na msemaji wa serikali Mohan Samaranayake alisema hana taarifa yoyote juu ya aliko rais huyo.

**WAANDAMANAJI WAKIOGELEA BAADA YA KUVAMIA MAKAZI RAIS**

Waandamanaji baadaye waliingia katika makazi ya kibinafsi ya waziri mkuu na kuyachoma moto, ofisi ya Wickremesinghe ilisema.

Haikubainika mara moja iwapo waziri mkuu huyo alikuwapo ndani wakati uvamizi huo ulipotokea.

Awali, maofisa wa polisi waliwarushia gesi ya kutoa machozi waandamanaji waliokuwa wamekusanyika katika makazi ya rais, wakipeperusha bendera na kuimba nyimbo.

Spika wa Bunge Mahinda Yapa Abeywardena, alisema katika taarifa yake kwa njia ya televisheni kwamba alimfahamisha Rajapaksa kwamba viongozi wa bunge walikutana na kuamua kuwa anafaa kuondoka madarakani na kwamba rais alikubali ombi lao.

Hata hivyo, Rajapaksa atasalia madarakani kwa muda kuhakikisha makabidhiano ya madaraka kwa njia ya amani, alisema Abeywardena.

"Aliniomba niwafahamishe wananchi kwamba atajiuzullu Jumatano ya tarehe 13, kwa sababu kuna haja ya makabidhiano ya madaraka kwa njia ya amani," Abeywardena alisema.

Mbunge wa upinzani Rauff Hakeem, alisema makubaliano yalifikiwa kwa spika wa bunge kukaimu nafasi ya rais.

*DW*



Waandamanaji wakiwa juu ya majengo ya Ikulu ya Rais wa Sri Lanka baada ya kuivamia juzi. **PICHA: BBC**

## Russia yashambulia jengo, sita wauawa

**KYIV, Ukraine**

WATU sita wameuawa na wengine 30 wanahofiwa kunasa kwenye vifusi baada ya makombora ya Russia kulipiga jengo la ghorofa tano katika eneo la Donetsk nchini Ukraine.

Gavana wa Donetsk, Pavlo Kyrylenko, alisema shambulizi hilo lilifanywa jana usiku katika mji wa Chasiv Yar.

Katika upande wa kusini, wanajeshi wa Ukraine walifyatua makombora katika maeneo ya Russia yakiwamo mabohari ya silaha katika eneo la Chornobaivka.

Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Marekani, Antony Blinken, akiwa ziarani Asia aliihimiza jamii ya kimataifa kuungana katika kulaani uchokozi wa Russia.

**CANADA ITATOA MTAMBO WA RUSSIA**

Serikali ya Canada itatoa mtambo muhimu uliotumika kusafirisha gesi kutoka Russia hadi Ujerumani ambao umekuwa nchini humo kwa matengenezo.

Awali mtambo huo uliorodheshwa kama sehemu ya vikwazo vilivyowekwa dhidi ya Russia.

Waziri wa maliasili Jonathan Wilkinson aliandika katika mtandao wake wa Twitter kwamba, baada ya mazungumzo na washirika wake wa Ulaya ikiwa ni pamoja na Ukraine na Ujerumani, Canada itatoa kibali cha muda cha mtambo huo wa Nord Stream 1 kwa Ujerumani. Mtambo huo ambao ulikuwa ukifanyiwa marekebisho nchini humo ulitakiwa kutumwa nchini Russia kama ilivyopangwa awali lakini sasa utasafirishwa hadi Ujerumani.

Hatua hiyo inatajwa itaisaidia Ulaya kuwa na gesi ya uhakika na nafuu wakati huu ambapo ikitafuta mbadala wa mafuta na gesi kutoka Russia.

**DW**

**Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Marekani, Antony Blinken, akiwa ziarani Asia aliihimiza jamii ya kimataifa kuungana katika kulaani uchokozi wa Russia.**

## Japan yapiga kura licha ya mauaji ya Abe

**TOKYO, Japan**

WANANCHI wa Japan wamefika vituoni kushiriki katika uchaguzi wa bunge ambao huenda Chama tawala cha Liberal Democratic (LDP) kikapata uungwaji mkono mkubwa baada ya kuuawa kwa waziri mkuu wa zamani Shinzo Abe.

Abe alikuwa mwanasiasa maarufu na mtu mwenye ushawishi katika maamuzi ya kisiasa.

Mtu anayetuhumiwa kuhusika na mauaji ya Abe ameiambia polisi kwamba alikusudia kutengeneza bomu. Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Japan vinaripoti kwamba mwanaume huyo ambaye alimpiga risasi Abe wakati akihutubia mkutano ijumaa katika kampeni mjini Nara.

Aliwaambia polisi kwamba alitengeneza bunduki nyingine nyingi.

Polisi ambayo ilifanya upekuzi katika makazi yake huko Magharibi mwa mji wa Nara ilizipata na kuzikamata bunduki zinazofanana na ile iliyopatikana eneo la tukio baada ya Abe kupigwa risasi.

*DW*

# KIPA WA AZAM KUTUA WAKATI WOWOTE

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Azam FC umesema muda wowote kuanzia leo wanatarajia kumpokea golikipa mpya ambaye anatokea Ulaya kwa lengo la kuboresha kikosi chao kuelekea msimu ujao pamoja na mashindano ya kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mtendaji mkuu wa Klabu hiyo, Abdul Karim Propat alisema msimu huu wanatarajia kuongeza wachezaji tisa ambapo kati yao watatu ni wakigeni na 6 ni wazawa.

"Tunatarajia kumpokea kipa wetu kati ya siku mbili hizi ambaye ataleta ushindani ndani ya timu yetu na wengine wawili watatoka nchi za Afrika Magharibi," alisema Karim.

Alisema mashabiki wao waendelee kuvuta subira watapata wachezaji ambao watafanya vizuri msimu huo.

Alisema wanatarajia kuipeleka timu yao Misri kwa ya kambi mapema ambayo itawasaidia kufanya vizuri msimu huo.

"Tunatarajia kwenda Misri kuweka kambi ya siku ishirini lengo ni kuhakikisha wachezaji wetu wanapata maandalizi ya muda mrefu."




Msanii wa sarakasi, Hassan Mkenjula, akionyesha umahiri wa kutembea juu kwa kutumia kamba wakati wa Maonyesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara katika viwanja vya Mwalimu Nyerere, barabara ya Kilwa, Dar es Salaam, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Manula ataka tuzo ya Afrika

**Na Saada Akida**

KIPA namba moja wa Simba, Aishi Manula, amesema kwa sasa anaumiza kichwa kuhakikisha anashindana na magolikia wa Afrika ili siku moja achukue tuzo ya kipa bora kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Manula misimu miwili iliyopita alitwaa tuzo ya kipa bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara na msimu huu tuzo hiyo imekwenda kwa kipa wa Yanga, Djigui Diarra.

Akizungumza na gazeti hili jana, Manula alisema kwa sasa mawazo na fikra zake ni kuhakikisha anafanya vizuri zaidi katika klabu yake ili kufikia malengo ya kuwa kipa bora Afrika.

Alisema ana imani atapambana kuhakikisha anasaidia timu yake kufanya vizuri katika michuano iliyopo mbele yao ikiwamo ya ndani na nje hasa katika michuano ya kimataifa ili kuja kutwaa tuzo hiyo.

"Niwapongeze wale wote waliofanya vizuri msimu huu na kutwaa tuzo kwa msimu huu, binafsi huu ni muda wa wengine, lakini kwa sasa ninachokifikiria zaidi ni kuhakikisha naisaidia timu yangu kufanya vizuri katika michuano iliyopo mbele yetu," alisema Manula. Alisema ana imani msimu ujao atafikia malengo hayo kwa sababu ya mikakati yao ni kuhakikisha wanafanya vizuri katika michuano hiyo na kufikia malengo yanayotarajiwa.

Simba inatarajiwa kuingia kambini kesho Jumanne na Julai 14 au 15 kikosi hicho kitaondoka nchini kuelekea Cairo, Misri kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu na michuano ya Kimataifa.

## Timu ya Taifa Taekwondo yaenda Rwanda

**Na Woinde Shizza, ARUSHA**

TIMU ya Taifa ya mchezo wa Taekwondo imeondoka nchini jana kuelekea Rwanda kwa ajili ya kushiriki mashindano ya ubigwa wa mchezo huo kwa nchi za Afrika yanayotarajiwa kuanza Julai 13 na kumalizika Julai 17 mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari mkurugenzi wa ufundi wa Shirikisho la Taekwondo Tanzania, Richard Kitolo alisema katika mashindano hayo nchi 40 kutoka Afrika zimethibitisha kushiriki.

Alisema kuwa maandalizi yamekamilika na wachezaji wote wapo vizuri kwa ajili ya kwenda kushiriki mashindano hayo.

Kwa upande wake kocha mkuu wa timu hiyo, Kim Keumloon alisema maandalizi ya wachezaji yamekamilika na wamefanya mazoezi ya kutosha na wanaimani watarudi na taji.

"Tumefanya mazoezi kwa kadri ya uwezo wetu na tunaamini tutashinda na kuleta ushindi nyumbani," alisema.

## Makata ashukuru kupunguziwa adhabu

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Mbeya Kwanza, Mbwana Makata, amesema anaishukuru Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania, kumkubalia msamaha wake na kumpunguzia adhabu ya kufungiwa cha miaka mitano hadi miezi sita.

Akizungumza na gazeti hili jana mara baada ya kupokea taarifa hizo Makata alisema anaishukuru Bodi hiyo kwa kuuthanini mchango wake kwenye mpira.

"Ninashukuru Bodi ya Ligi Kuu kwa kusikiliza msamaha wangu na kunipunguzia adhabu wametambua mchango wangu kwani tangu nianze kufundisha mpira miaka ya 1998 nilifanikiwa kupandisha timu nying," alisema Makata.

Alisema baada ya kupunguziwa adhabu hiyo moja kwa moja atakaa na kutafakari nini afanye kwa kile ambacho kilimkuta mpaka kupatikana na kosa hilo ambalo amekiri kumtia doa.

"Ninawasihi makocha wenzangu wajifunze kupitia kosa langu ninawashauri wafuate kanuni na taratibu za mpira," alisema.

Alisema adhabu yake ilianza Mei 16, hivyo mpaka sasa imebaki miezi mitatu amalize. Mbwana Makata pamoja na Meneja wake David Naftali walipewa adhabu hiyo baada ya kuhusishwa na kosa la kuishawishi timu yake isicheze na timu ya Namungo FC.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**TIELEMANS HUYO ARSENAL**
KLABU ya Arsenal ina uhakika wa kuipiku Manchester United kwenye usajili wa pauni milioni 30 wa kiungo wa kati wa Leicester na Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25. ***(Sun)***

**ANTONY NA MAN**
KLABU ya Manchester United wametoa dau la pauni milioni 51 kumnunua mshambuliaji wa Ajax Mbrazil Antony mwenye umri wa miaka 22, lakini klabu hiyo ya Uholanzi inashikilia dau la pauni milioni 68. ***(Goal)***

**NUNES KUNUNULIWA**
CHELSEA inaandaa dau la pauni milioni 38 kumnunua kiungo wa kati wa Sporting Lisbon na Ureno, Matheus Nunes, ambaye analengwa na Wolves. ***(A Bola)***

**RICHARDS ATAKIWA FOREST**
KLABU ya Nottingham Forest inatumaini kukamilisha mikataba ya mlinzi wa kushoto wa Bayern Munich, Omar Richards mwenye umri wa miaka 24, na mlinzi wa kulia wa Liverpool, Neco Williams wa Wales mwenye umri wa miaka 21, ifikapo wikendi. ***(Athletic)***

**WILLIAMS AWANIWA**
KLABU ya Southampton pia wanavutiwa na Neco Williams na wanatumaini kumpiku Nottingham Forest kwenye saini ya beki huyo. ***(Football Insider)***

**GORDON NA MKATABA**
KLABU ya Everton inajiandaa kumpa mkataba mpya winga wa England, Anthony Gordon mwenye umri wa miaka 21 ili kuzuia nia ya Newcastle. ***(Times)***

**LEWIN KUBAKI**
KLABU ya Everton pia haina haja ya kumuuza mshambuliaji wa England, Dominic Calvert-Lewin na wanaweza kumpa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 mkataba mpya pia. ***(Mirror)***

**RAPHINHA OFA YA MWISHO**
LEEDS United wamewataka Barcelona kutoa ofa ya mwisho kwa Raphinha wiki hii kwani wanataka mustakabali wa mshambuliaji huyo wa Brazili kutatuliwa haraka iwezekanavyo. ***(Sport)***

**WHITE ATAKIWA**
KLABU ya Crystal Palace wana matumaini ya kuzishinda Everton na Nottingham Forest katika kumnasa kiungo wa kati wa Wolves, Morgan Gibbs-White mwenye umri wa miaka 22. ***(Talksport)***

**DOWNES AWANIWA**
CRYSTAL Palace wako kwenye mazungumzo ya kumsajili kiungo wa kati wa Swansea, Flynn Downes mwenye umri wa miaka 23, kwa pauni milioni 8. ***(Mail)***

**ARSENAL KUUZA SABA**
ARSENAL wanataka kuuza wachezaji saba akiwamo winga wa Ivory Coast na aliyesajiliwa kwa rekodi ya klabu, Nicolas Pepe mwenye umri wa miaka 27.

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND APEWA JEZI NAMBA 9 MAN CITY

Anairithi kutoka kwa Jesus ambaye ametimkia Arsenal...

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City imethibitisha kuwa mchezaji aliyesajiliwa kwa fedha nyingi msimu huu wa joto, Erling Haaland atavaa jezi namba tisa iliyoachwa hivi karibuni na Gabriel Jesus.

City ilitangaza dili la kumnunua Haaland kuanzia Mei, lakini mashabiki walikuwa wameachwa wakikisia ni jezi gani ambayo raia huyo wa Norway angevaa.

Jesus amekamilisha uhamisho wake wa pauni milioni 45 kwenda Arsenal katika siku za hivi karibuni, na kuachia jezi namba tisa ambayo mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alikuwa anavaa tangu mwaka 2019.

Kabla ya Jesus, City ambao ni mabingwa mara nne wa Ligi Kuu England, jezi namba tisa ilivaliwa na wachezaji Nolito, Alvaro Negredo, Emmanuel Adebayor, Valeri Bojinov, Emile Mpenza, Paolo Wanchope na Andy Cole.

Haaland alivaa namba tisa kwa misimu miwili akiwa na klabu ya zamani ya Borussia Dortmund, ambapo alitoka kuvaa namba 17.

Hapo awali alikuwa anavaa jezi namba 30 katika Red Bull Salzburg na Molde.

Mashabiki wa City wana matarajio makubwa ya Haaland msimu ujao na zaidi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 alikuwa akiifuata klabu hiyo kutokana na muda wa baba yake kuwa mchezaji na anafika akiwa na rekodi nzuri ya kufunga mabao ambayo imemfanya kufunga mabao 135 katika michezo 137 kwa klabu na nchi tangu majira ya joto mwaka 2019.

Juu ya Haaland, City pia wamekamilisha usajili wa Kalvin Phillips kutoka Leeds United.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England tayari alikuwa amepewa jezi namba nne aliyokuwa akivaa Vincent Kompany.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
SKEID FOTBALL
VERSUS
BRYNE
1 | 2.28
X | 3.43
2 | 2.70

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP HAKUHOFU KUHUSU SALAH KUONDOKA



**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp hakuwahi kuwa na wasiwasi kuhusu uwezekano wa kuwapoteza Sadio Mane na Mohamed Salah kwa sababu ilikuwa “wazi kila wakati” kwamba watabakia Liverpool.

Mustakabali wa Mane na Liverpool ulikuwa shakani, huku tetesi zikidai kuwa yuko tayari kuondoka akiwa amebakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake.

Mwishowe, uhamisho wake wa euro milioni 41 kwenda Bayern Munich ulitimia haraka sana Juni baada ya Liverpool kupata saini ya Darwin Nunez kutoka Benfica.

Lakini uamuzi wa Mane kuondoka, wakati huo, ulizua wasiwasi miongoni mwa mashabiki wa Liverpool kwa sababu Salah pia alikuwa na miezi 12 tu ya kumaliza mkataba wake.

Uvumi ulienea kwamba, mazungumzo ya mkataba mpya na Salah yamekuwa yakisuasua kwa muda, lakini hatimaye ilitangazwa Julai 1 kwamba, nyota huyo wa Misri alisaini mkataba mpya ambao utaendelea hadi Juni 2025.

Licha ya hali ya mazungumzo kuonekana kuwa ya muda mrefu, Klopp anasisitiza kuwa kila mara alikuwa ametulia kuhusu mustakabali wa Salah.

“Nilijua ingefanyika, ilikuwa wazi kila wakati Mo anataka kubaki,” alisema Klopp akiiambia tovuti rasmi ya Liverpool.

“Nilizungumza naye kwa uwazi na ilikuwa wazi kila wakati: ‘Nataka kubaki.’ Lakini ni mkataba muhimu, mambo tofauti yanapaswa kuzingatiwa na hiyo ndiyo inachukua muda wakati mwingine.

“Hatuwezi kutimiza matarajio kutoka kwa ulimwengu wa nje kila wakati - ‘kuna mkataba unaoisha, mwaka ujao utamalizika, kwa hivyo suluhisha sasa.’

“Mambo yanahitaji muda, lakini ni wazi tuna uzoefu wa kutosha kukabiliana na aina hii ya mambo. Ana furaha kubwa sasa anaweza kuongeza muda wake hapa.

“Tuna furaha sana, mchezaji wa kiwango cha kimataifa. Hebu fikiria unapaswa kumsajili Mo Salah sasa; yuko katika klabu nyingine na unataka mchezaji mwenye namba alizotengeneza kwa miaka mingi. Haiwezekani, lakini tunaye na anataka kubaki.”

# Wenger aunga mkono Wilshere kustaafu

**LONDON, England**

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger ameunga mkono uamuzi wa Jack Wilshere kustaafu soka akiwa na umri wa miaka 30 pekee, na kuutaja kuwa ‘uamuzi sahihi’.

Wilshere alitoa tangazo hilo kupitia mitandao ya kijamii Ijumaa, akiamua kumalizia soka lake baada ya kumalizika kwa mkataba wake wa muda mfupi na klabu ya AGF ya Denmark.

Mchezaji huyo hapo awali alichezea Bournemouth mechi 14 katika kipindi cha pili cha msimu wa 2020/21 baada ya kumaliza mkataba wake na West Ham miezi michache iliyopita.

Wilshere alijipambanua kwenye soka mwaka 2008 akiwa na umri wa miaka 16 tu, lakini majeraha yalikuja kuzorotesha kipaji chake.

Alijidhihirisha kama mchezaji muhimu wa kikosi cha kwanza kwa Arsenal chini ya uangalizi wa Wenger msimu wa 2010/11 akiwa bado kijana, akicheza mechi 49 katika mashindano yote. Hata hivyo, majeraha ya kifundo cha mguu kabla ya msimu mpya yalimfanya kuwa nje ya msimu mzima wa 2011/12 na bila shaka uchezaji wake haukuweza kupona.

“Alikuwa jasiri, alikuwa na kipaji, hakuwa na hofu na mtu yeyote. Ndio maana tulifikiri angeweza kuanza akiwa na umri mdogo sana. Moja kwa moja alionyesha kuwa ana uwezo wa kuwa mchezaji mkuu,” alisema Wenger kuhusu Wilshere katika mahojiano na Sky Sports.

“Alikuwa na kipaji cha kipekee, lakini hakucheza michezo ya kutosha kwa sababu ya majeraha na mwishowe ndio maana alilazimika kuacha. Ni vigumu sana kwa nyota kama ilivyokuwa wakati huwezi kucheza kwa ubora wako tena. Hiyo ni ngumu kumeza. Ndio maana nadhani amefanya uamuzi sahihi.”

Wilshere anatarajiwa mara moja kuanza kazi ya ukocha katika timu ya Arsenal ya vijana chini ya umri wa miaka 18.

HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA

# DODOMA JIJI YAENDELEA KUKIMBIZA USAJILI

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Dodoma Jiji imeonekana kutotaka kurudia makosa ya msimu uliopita, baada ya kuendelea na zoezi la usajili mfululizo, ambapo ilimtangaza Paul Peter kutoka Azam FC kuwa mchezaji wao rasmi.

Hiyo ni siku moja tu baada ya kunyaka saini ya straika Randy Bangala, ambaye ni mdogo wa kiungo mkabaji wa Yanga, Yannick Bangala kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Katibu Mtendaji wa klabu hiyo Fortunatus John amesema mbali na kusajili, klabu hiyo inawaongezea mikataba wachezaji ambao inawahitaji kuendelea nao kwa msimu ujao wa Ligi Kuu.

"Tunaendelea kusajili kama unavyoona, lakini tunawaongezea mikataba wachezaji ambao benchi la ufundi litaendelea nao kwa msimu ujao." Alisema.

Wachezaji ambao imewaongezea mikataba mpaka sasa ni nahodha Mbwana Kibacha, na Gerald Mgeveke.

Tayari klabu hiyo imeshawasajili wachezaji Collins Opare raia wa Kenya na Mghana Christian Zigah, wote kutoka Biashara United ambayo tayari imeshuka daraja.

Kutokana na usajili huo, Dodoma Jiji imebakisha jumla ya wachezaji sita ili kumaliza idadi wanayohitaji kusajili msimu huu.

Katibu Mtendaji huyo alisema kuwa wanatarajia kusajili wachezaji 10 na kuacha idadi hiyo hiyo kwa ajili ya msimu ujao baada ya kutofanya vema msimu uliopita ikimaliza ikiwa kwenye nafasi ya 11 na pointi 35.



Baadhi ya wajumbe wa matawi wa Klabu ya Yanga, wakipiga kula kuchagua viongozi wa klabu hiyo wakati wa uchaguzi mkuu uliofanyika katika jengo la mikutano la Kimataifa la Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga yachelewa, Coastal yafukia kitu

Na Adam Fungamwango

KLABU za Yanga na Coastal Union zimepewa onyo kali na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu kutokana na kukiuka kanuni mbalimbali zinazoendesha mpira wa miguu, moja ikionywa kwa uchelewaji na nyingine kuchimba na kufukia kitu kisichojulikana uwanjani.

Yanga imepewa onyo kwa uchelewaji kwani ilishindwa kufika kwa wakati husika kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Coastal Union, huku Coastal nao wakipewa pia onyo kwa kufukia kuchimba na kufikia kitu kisichojulikana uwanjani, kuashiria mambo ya kishirikina kwenye mechi ya dhidi ya Namungo FC.

Taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi imesema, katika kikao chake cha Julai 6 mwaka huu, ilipitia mwenendo wa matukio mbalimbali ya Ligi Kuu na kufanya maamuzi hayo.

"Mechi namba 214, Yanga ilicheza dhidi ya Coastal na kushinda mabao 3-0. Kwenye mechi hiyo Yanga imepewa onyo kali kwa kosa la kuchelewa kuwasili uwanjani. Ilifika saa 1:12 usiku badala ya saa 1:00 usiku kuelekea mchezo tajwa uliochezwa Mei 15, 2022 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Adhabu hiyo ni kwa uzingativu wa kanuni 17: (15 & 60) ya Ligi Kuu kuhusu taratibu za mchezo." Ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo pia imesema kwenye mechi namba 217, ambayo Coastal Union ilishinda bao 1-0 ugenini kwenye Uwanja wa Ilulu, mchezaji Bigirimana Blaise wa Namungo FC, amepewa onyo kali kwa kuonekana akitupa vipande vya ndimu kwenye upande ilipokaa timu ya Coastal, huku mchezaji mwenzake Hamisi Mgunya naye akipewa onyo kwa kosa la kwenda kwenye goli la Coastal Union na kumwaga kiminiminika kutoka kwenye chupa kuelekea mchezo huo uliochezwa Juni 20, 2022.

"Pia klabu ya Coastal Union imepewa onyo kali kwa kosa la wachezaji wake kuzingira eneo la katikati ya uwanja na kuchimba shimo dogo, kisha kufukia kitu kisichojulikana.

Adhabu hii ni kwa uzingativu wa kanuni ya 47 (1) ya Ligi Kuu kuhusu udhibiti wa klabu." Ilimaliza taarifa hiyo ya Bodi ya Ligi.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 11/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1147 | Henan Jianye vs Changchun Yatai | 2.40 | 3.19 | 2.70 |
| 14:30 | 1822 | Shenzhen vs Beijing Guoan | 3.29 | 3.29 | 2.03 |
| 14:30 | 4735 | Hebei Zhongji vs Guangzhou Evergrande | 3.73 | 3.39 | 1.86 |
| 16:00 | 1225 | Velez Sarsfield Reserve vs Colon de Santa Fe Reserve | 2.23 | 3.25 | 2.90 |
| 16:00 | 5772 | Huracan Reserve vs CA Lanus | 2.29 | 3.25 | 2.81 |
| 18:00 | 2699 | Ilves Tampere vs AC Oulu | 1.67 | 3.69 | 4.33 |
| 18:30 | 2508 | FC KTP vs KPV Kokkola | 1.51 | 4.14 | 5.12 |
| 18:30 | 3603 | Japs vs IF Gnistan | 3.39 | 3.49 | 1.93 |
| 18:30 | 3808 | Kerho 07 vs MP Mikkeli | 2.19 | 3.49 | 2.80 |
| 18:30 | 4374 | PFC Spartak Varna vs Slavia Sofia | 3.00 | 3.10 | 2.25 |
| 19:00 | 1295 | Fredrikstad vs Kongsvinger IL | 1.99 | 3.58 | 3.14 |
| 19:00 | 1633 | Mjondalen vs Aasane Fotball | 1.73 | 3.78 | 3.88 |
| 19:00 | 2076 | Fana vs Brann 2 | 2.13 | 3.86 | 2.69 |
| 19:00 | 3223 | Skeid Fotball vs Bryne | 2.28 | 3.43 | 2.70 |
| 19:00 | 3284 | Brodd vs Viking FK 2 | 2.59 | 3.62 | 2.28 |
| 19:00 | 3938 | Kfum Oslo vs IK Start | 2.55 | 3.53 | 2.36 |
| 19:00 | 4370 | Austria W vs Northern Ireland W | 1.15 | 6.47 | 13.71 |
| 19:00 | 4455 | Sogndal vs Grorud IL | 1.61 | 4.13 | 4.22 |
| 19:30 | 2207 | Aalesund 2 vs Hodd 2 | 1.12 | 7.85 | 12.75 |
| 19:30 | 4339 | Molde FK 2 vs Spjelkavik | 1.52 | 4.42 | 4.61 |
| 20:00 | 1101 | Hammarby vs IFK Goteborg | 1.60 | 3.72 | 4.89 |
| 20:00 | 1171 | Bremnes vs FK Haugesund 2 | 1.45 | 4.83 | 4.93 |
| 20:00 | 2856 | Lysekloster vs Sandnes Ulf 2 | 1.60 | 4.54 | 3.94 |
| 20:00 | 3425 | IFK Varnamo vs GIF Sundsvall | 1.49 | 4.03 | 5.50 |
| 20:00 | 3475 | IK Brage vs AFC Eskilstuna | 1.83 | 3.72 | 4.07 |
| 20:00 | 3903 | Nordstrand vs Stabaek Fotball 2 | 1.21 | 6.26 | 8.61 |
| 20:00 | 4555 | Raufoss IL 2 vs Elverum | 8.07 | 5.90 | 1.24 |
| 20:00 | 5656 | Helsingborg vs Djurgardens IF | 5.12 | 3.89 | 1.54 |
| 20:45 | 5382 | Beroe vs Botev Vratsa | 1.78 | 3.44 | 4.03 |
| 21:00 | 3609 | Kolubara vs FK Radnicki 1923 | 2.25 | 3.23 | 2.89 |
| 21:00 | 3917 | Sport Boys Association vs UTC Cajamarca | 2.17 | 3.28 | 2.99 |
| 21:30 | 3047 | CA Fenix vs Villa San Carlos | 3.54 | 2.85 | 2.14 |
| 21:30 | 5381 | Sportivo Barracas vs Club Mercedes | 1.74 | 3.29 | 4.52 |
| 22:00 | 1713 | England W vs Norway W | 1.68 | 3.68 | 4.31 |
| 22:15 | 1213 | Stjarnan vs Leiknir | 1.62 | 3.92 | 4.41 |
| 22:15 | 3374 | Fram Reykjavik vs Hafnarfjordur | 3.28 | 3.68 | 1.91 |
| 22:15 | 5691 | Valur vs Keflavik IF | 1.46 | 4.43 | 5.32 |
| 23:00 | 2359 | Orsomarso vs Deportes Quindio | 4.11 | 3.01 | 1.90 |
| 23:15 | 4311 | Escuela Municipal Deportivo Binacional vs Univ San Martin | 1.32 | 4.70 | 7.64 |
| 23:35 | 4488 | Defensores Belgrano vs Atletico Rafaela | 2.05 | 2.99 | 3.62 |

JUMANNE - 12/07/2022

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 3271 | Paraguay W vs Chile W | 7.05 | 4.70 | 1.34 |
| 01:00 | 1482 | Union Espanola vs Universidad Catolica | 2.42 | 3.23 | 2.65 |
| 01:00 | 1882 | Colon Santa Fe vs Velez Sarsfield | 2.85 | 3.00 | 2.40 |
| 01:00 | 5696 | Defensa Justicia vs Aldosivi | 1.60 | 3.49 | 5.30 |
| 01:30 | 5104 | CS Cerrito vs Cerro Largo FC | 3.04 | 2.99 | 2.29 |
| 01:40 | 4472 | Atletico Alvarado vs Almirante Brown | 2.31 | 2.90 | 3.10 |
| 02:00 | 1311 | Panama W vs Trinidad And Tobago W | 1.42 | 4.23 | 6.30 |
| 02:00 | 1341 | ABC RN vs Manaus Fc/Am | 1.89 | 3.05 | 4.13 |
| 02:00 | 5581 | Canada W vs Costa Rica W | 1.12 | 7.29 | 13.79 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Julai 11, 2022
Nipashe



## Haaland apewa jezi namba 9 Man City



Mchezaji mpya wa timu ya Yanga, Gael Bilimana (kushoto), akizungumza mbele ya wajumbe wa matawi wa klabu hiyo katika mkutano wa uchaguzi mkuu uliofanyika jijini Dar es Salaam juzi (katikati) ni Rais wa Yanga, Injinia Hersi Said na kulia ni mhamasishaji wa klabu hiyo, Hajji Manara. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MSUVA KUFUNGA USAJILI YANGA

●●●Hersi atamba kwamba, mtoto anarudi nyumbani, huku Aziz Ki akitarajiwa...

**Na Saada Akida**

KLABU ya Yanga inatarajia kufunga usajili wake kwa kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Simon Msuva kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye kikosi hicho kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa mujibu wa rais mpya wa klabu ya Yanga, Hersi Said, akizungumza kwa mafumbo, alisema watafunga usajili kwa kumrejesha mtoto wao nyumbani.

Hersi alisema wanafanya usajili kulingana na mapendekezo ya kocha mkuu Nesredine Nabi kwa mchezaji wanayewahitaji akiwemo Msuva ambaye ni mzawa anayerudishwa Yanga.

Hersi alisema hayo juzi katika uchaguzi mkuu wa Yanga, baada ya kutangazwa kuwa rais wa klabu hiyo na kumtambulisha kiungo, Geal Bigirimana.

Utambulisho huo, uliwafanya Yanga kufikisha wachezaji watatu ambao imewatambulisha hadi sasa wakiwamo, Lazarous Kambole na Benard Morrison.

Hersi alisema usajili uko vizuri kwa asilimia kubwa wamekamilisha kila kitu na zimebaki nafasi chache ambazo zinaendelea kufanyiwa kazi ikiwamo kukamilisha usajili wa mchezaji mzawa.

"Kila kitu kipo vizuri, tayari usajili umekamilika kwa asilimia kubwa na baadhi ya nafasi tunakamilisha, kuhusu mchezaji mzawa, hilo tumefanya kile alichokipendekeza kocha Nabi, kwa kumrejesha mtoto wetu nyumbani (Msuva) waliosema harudi niwahakikishie kwamba mtoto anarudi kwao," alisema Hersi.

Mbali na Msuva, Hersi alisema muda wowote kuanzia sasa watatambulisha mchezaji mwingine mwa kimataifa (beki wa kushoto Joyce Lomalisa Mutambala) kuwa sehemu ya wachezaji watano wa kigeni waliosajiliwa kwa ajili ya kuimarisha kikosi cha timu hiyo.

Mutambala anajiunga Yanga akitokea Bravos do Maqui ya Angola, pia amewahi kucheza GD Interclube (Angola), AS Vita (DR Congo) na Mouscron ya Ubelgiji.

Alisema wanasajili wachezaji wazuri na ndio maana wamemchukua mchezaji wa zamani wa klabu ya Newcastle iliyokuwa inashiriki Ligi Kuu nchini England.

"Sisi tunasajili na tumeahidi kabisa kushusha vifaa, huyu hajacheza timu ndogo bali amecheza timu kubwa na kwenye ligi kubwa. Wanasema eti Fiston Mayele ataenda Kaizer Chiefs, sisi wenyewe tunachukua wachezaji kwao huko," alisema Hersi.

Alisema kuna mchezaji walimtambulisha na mwingine atаingia leo Jumatatu kutambulishwa rasmi kwa sababu wanahitaji kuimarisha timu hiyo kwa msimu ujao.

"Yule mchezaji (Stephen Aziz Ki) anasubiriwa na Wanayanga niwahakikishie anatua nchini kesho Jumatatu (leo) na kuwa sehemu ya usajili ambao tumefanya kwa wachezaji ambao wametakiwa na Kocha Nabi kwa ajili ya kuimarisha kikosi cha timu yetu."

## Akpan wa Coastal atua rasmi Simba

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba jana mchana imemtambulisha rasmi kiungo mkabaji, mwenye uwezo pia wa kucheza kama kiungo mshambuliaji raia wa Nigeria, akitokea kwenye klabu ya Coastal Union.

Zilikuwa ni tetesi za muda mrefu huku zikithibitishwa na Coastal Union wenyewe, lakini klabu hiyo ilikuwa kimya kwa muda mrefu, hadi jana ilipoamua kumweka bayana.

Kwenye mtandao wao rasmi ya Instagram, klabu hiyo ilitoa picha ya mchezaji huyo na kuandika maneno ya kumkaribisha, pamoja na kumpa sifa lukuki.

"Kiungo wa katikati ya dimba mwenye uwezo mkubwa wa kuhimili mechi za aina zote. Victor Akpan ni Mnyama." Ulindika mtandao wa klabu hiyo.

Misimu kadhaa iliyopita, mchezaji hiyo aliwahi kwenda kufanya majaribio na timu hiyo, lakini hakuweza kufanikiwa na baada ya hapo alikwenda Zanzibar kujiunga na klabu mbalimbali za Ligi Kuu, kabla ya Coastal Union kumuona na kumsajili.

Anakuwa ni mchezaji wa tatu mpya kutambulishwa na klabu hiyo ambayo msimu huu imeahidi kukijenga upya kikosi chake ambacho hakikufanya vema na kupoteza mataji yote iliyokuwa inashikilia.

Moses Phiri raia wa Zambia ndiye aliyekuwa mchezaji wa kwanza wa Simba kutangazwa msimu huu, na baada ya hapo kilizuka kimya kilichowatisha wanachama na mashabiki wa klabu hiyo, kabla ya juzi kuanza tena kutambulisha wachezaji, ikianza na straika wa zamani wa Mbao FC, Singida United, na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, Habib Kyombo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, alibainisha kuwa ukimya wao si kama walikuwa hawasajili kama wengi wanavyodhani, ila ni mpango mkakati wa kuzifanya taarifa zao za usajili ziwe hitaji kwa watu wengi kwa ajili ya klabu kujiingizia kipato. "Kwa wenzetu utambulisho wa mchezaji ni biashara, siku ya utambulisho hurejesha sehemu ya gharama za usajili na mauzo ya jezi. Sisi bado hatujafikia huko lakini ni lazima tuanze kidogo kidogo kufanya biashara ya utambulisho wa wachezaji," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >